**11 JUNI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Arobaini na Nne – Tarehe 11 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**MHE. MUSSA A. ZUNGU – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KANUNI ZA BUNGE:**

Azimio la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni za Bunge kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Bunge.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 561

### Watumishi wa Afya Wanaotakiwa katika Kituo cha Afya au Zahanati

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza: -

Je, watumishi wangapi wa afya wanatakiwa katika zahanati au kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mwongozo wa Wizara ya Afya wa mwaka 2014 – 2019 umeainisha idadi ya watumishi wa kada ya afya wanaohitajika katika ngazi ya zahanati kuwa ni 15 - 20 na kituo cha afya watumishi kati ya 39 – 52. Aidha, idadi hii inaweza kupungua au kuongezeka kulingana na idadi ya wagonjwa wanaopata huduma katika kituo husika.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI inakamilisha kuhuisha Mwongozo wa Ikama ya Watumishi wa Sekta ya Afya kwa ngazi ya huduma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kyerwa yenye *population* ya watu 400,000 kwa mujibu wa Sensa za mwaka 2022. Pia ina zahanati 24 badala ya 99 kama mwongozo unavyoonesha, ikiwa na vituo vya afya vitano badala ya vituo 24 kwa mujibu wa kata zake 24.

Swali langu ni kwa nini kulingana na *population census*, ni kwanini hatuna zahanati za kutosha kulingana na mwongozo wa Serikali kama ilivyo vituo vya afya?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, wastani wa wataalam katika vituo vya afya kwa Wilaya ya Kyerwa ni watatu mpaka watano kwa zahanati, na vituo vya afya ni 15 mpaka 20. Swali langu, ni kwa nini tumeshindwa kupeleka watumishi wa kutosha tunakuwa sasa na *deficit* ya watumishi 70% kwa Wilaya ya Kyerwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza ninaomba nianze kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi wa mwaka 2007 – 2017, mpango ulikuwa ni kujenga zahanati kila kijiji na kila mtaa na kujenga kituo cha afya kila kata, lakini Serikali ilifanya mapitio ya mwongozo huo wa 2007 – 2019 na kuona uhalisia wake, kwa sababu hakukuwa na uhalisia wa kuwa na zahanati kwenye kila kijiji na kila mtaa, lakini hakuna uhalisia wa kuwa na kituo cha afya kwenye kila kata katika kata zote hapa nchini na ndiyo maana tulikuja na mwongozo wa kujenga zahanati katika vijiji ambavyo vina idadi ambayo angalau vinatosheleza kigezo cha idadi ya wananchi, lakini pia kujenga vituo vya afya kwenye kata za kimkakati na siyo kila kata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jambo la kwanza Mheshimiwa Theonest, ninaomba nikupe msisitizo huo kwamba hatujengi kituo cha afya kwenye kila kata wala kila kijiji ila vijiji na kata za kimkakati, lakini ninafahamu kwamba katika Jimbo la Kyerwa bado kuna upungufu wa vituo vya afya na tayari halmashauri

imekwishawasilisha kata za kimkakati na Serikali imeanza kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Anatropia na wananchi wa Jimbo la Kyerwa kwamba Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan itaendelea kupeleka fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la pili, idadi ya watumishi kwenye zahanati au vituo vya afya mwongozo umetolewa kwa ujumla wake, lakini zahanati hizi zinatofautiana idadi ya wagonjwa ambao wanatibiwa, zipo zahanati ambazo zinatibu wagonjwa siyo zaidi ya 10 kwa siku nzima. Kwa hiyo, zahanati kama hii ikiwa na watumishi watatu wanatosha kabisa kutoa huduma kwa wagonjwa ambao wanatibiwa kwa uchache katika zahanati hizo, lakini zipo zahanati ambazo zinatibu wagonjwa zaidi ya 100 na zaidi na hizi zinakuwa na watumishi wengi zaidi na hivyo hivyo vituo vya afya vinatofautiana.

Mheshimiwa Spika, msingi wa kupeleka watumishi wa afya ni idadi ya wagonjwa wanaotibiwa kwa siku katika kila kituo. Kwa hiyo, nikuhakikishie, tunafahamu kuna upungufu wa watumishi, lakini Mheshimiwa Rais ameendelea kuajiri na katika kipindi cha miaka hii minne jumla ya watumishi 34,720 wa sekta ya afya wameajiriwa na Kyerwa wamepelekwa na tutahakikisha kwamba tunaendelea kupeleka watumishi hao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Kijiji cha Ibofwi kilichopo katika kata ya Ilole, Wilaya ya Kilolo hakina zahanati na hata Kata ya Ilole haina kituo cha afya, wananchi wanatoka umbali mrefu sana. Ninamshukuru sana, jana Waziri Mheshimiwa Jerry alikuwa kwenye ziara na walimpa hii taarifa, wananchi ni wengi lakini wanapata mateso makubwa barabara pia hazipitiki.

Je, lini sasa zahanati hii itajengwa kwa sababu zaidi ya miaka 15 inajengwa lakini haikamiliki? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba vipo vijiji na kata abazo zinakidhi vigezo vya kuwa na zahanati au vituo vya afya na Serikali imeendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa zahanati katika maeneo hayo, lakini pia ujenzi wa vituo vya afya katika kata hizo.

Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba Serikali imekwishaanza na katika kata ya Ukumbi katika Jimbo la Kilolo, hivi karibuni Mheshimiwa Rais amepeleka zaidi ya shilingi milioni 623 na kata nyingine na zahanati nyingine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge safari ni hatua, tukuhakikishie kwamba, Serikali itaendelea kupeleka fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimewaona, ninaona mmesharejea tena kwenye michango wakati wa kuuliza swali, nenda moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Stella Fiyao swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana, ni lini Serikali mtajenga kituo cha afya katika Kata ya Mbebe iliyopo ndani ya Wilaya ya Ileje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kata ya Mbebe katika Wilaya ya Ileje ni moja ya kata ambazo zinakidhi vigezo na tayari tumeziingiza kwenye mpango wa Benki ya Dunia kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Songambele ni miongoni mwa kata za kimkakati ambazo niliziombea fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Ni lini shilingi milioni 250 zitaletwa ili kituo cha afya kianze kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishatenga shilingi bilioni 30 kwa ajili ya majimbo 120 awamu ya kwanza, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwa kuanza na shilingi milioni 250 na mpaka leo karibu majimbo yote 120 yamekwishapelekewa shilingi milioni 250 na baada ya hapa nitafuatilia kuona Kituo cha Afya cha Songambele katika Jimbo la Kyerwa kama kipo awamu ya pili, basi fedha zitapelekwa awamu ya pili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Simike, Kata ya Lufingo Wilaya ya Rungwe, wananchi wameweza kujitahidi kujenga zahanati. Ni lini Serikali mtatuongezea nguvu ili kuweza kumaliza na kiweze kuanza kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita Serikali imepeleka fedha katika maboma wastani matatu kila jimbo na kila halmashauri kwa ajili ya umaliziaji wa maboma ya zahanati. Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kuona kama boma hilo limepelekewa fedha na kama halijapelekewa fedha nikuhakikishie tu wewe na wananchi wa Jimbo la Rungwe

kwamba, Serikali hii itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kukamilisha maboma hayo ya zahanati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, Mheshimiwa Mariam Kisangi kwa niaba yake.

Na. 562

**Halmashauri Kutenga Asilimia 60 Kuboresha Barabara**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itazielekeza halmashauri kutenga 60% ya mapato ya ndani kuboresha miundombinu ya barabara za ndani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara katika kuleta maendeleo na kupunguza kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaendeshwa kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura 287 (Mamlaka za Wilaya) na Sura 288 (Mamlaka za Miji). Sheria hizo zimetoa mamlaka kwa halmashauri kupanga vipaumbele vyake na matumizi ya fedha katika halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa miongozo kunapokuwa na uhitaji wa kufanya hivyo ambapo kwa sasa utengaji wa fedha kwa ajili ya uboreshaji wa barabara za ndani ni 10% ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa halmashauri zinazochangia 70% kwenye miradi ya maendeleo zikiwemo halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kubuni na kuongeza vyanzo vya mapato na kuweza kukusanya na kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali inaonyesha wazi kwamba imetenga 10% kwa ajili ya utengenezaji wa barabara, lakini katika Mkoa wa Dar es Salaam hususani katika Jimbo la Segerea kumekuwa na changamoto kubwa ya barabara za mitaani.

Je, Serikali sasa haioni haja ya kurekebisha sheria hiyo na kuongeza, kwa sababu kipaumbele cha Mkoa wa Dar es Salaam ni kupata barabara bora, Serikali haioni haja ya kufanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa katika Jimbo la Segerea katika Kata za Tegeta, Bonyokwa, Liwiti, Kipawa na kata nyingine nyingi za Jimbo la Segerea halijawa na barabara za lami hali ambayo inaleta sintofahamu sana katika jimbo hilo. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha ule mradi wa *DMDP* unaanza mara moja ili kuwasaidia wananchi hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba katika Majiji na Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam, lakini na maeneo mengine ya miji na majiji kipaumbele cha barabara ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali, lakini pia ni moja ya mahitaji makubwa ya wananchi. Nimhakikishie Mheshimiwa mama yangu Mariam Kisangi kwamba Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara za mijini zinaboreshwa kupitia *TARURA*, lakini

pia kupitia *DMDP* kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie tu kwamba ile 10% kwa Manispaa na Jiji la Dar es Salaam ni kiwango cha chini angalau 10% lakini Manispaa au Jiji lina uwezo wa kutenga zaidi ya 10% kulingana na uhitaji wa barabara katika Manispaa husika.

Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwasisitiza Wakurugenzi wote wa Majiji na Manispaa na hususani ya Mkoa wa Dar es Salaam kuhakikisha kwamba wanatenga fedha angalau zinazotosheleza kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusiana na ujenzi wa barabara za lami; Mradi wa *DMDP* unaendelea katika Mkoa wa Dar es Salaam katika maeneo mbalimbali katika Jiji la Ilala kwa maana ya Jiji la Dar es Salaam, lakini pia na Manispaa zake na tutaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba *TARURA* pia wanajenga barabara za lami, lakini pia *DMDP* na miradi mingine yote ya Serikali ili kuboresha barabara katika Mkoa wa Dar es Salaam.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda nimekuona, lakini ninaona una swali hapa linafuata baada ya hili, na kwa sababu hakukuwa na Mbunge mwingine aliyesimama zaidi yako, Mheshimiwa Joseph George Kakunda Mbunge wa Sikonge sasa aulize swali lake.

Na. 563

**Kukosa Huduma ya Maji Mashuleni**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza: -

Je, lini tatizo la kukosa huduma ya maji kwenye shule za msingi na sekondari zenye vyoo vya kisasa litatatuliwa lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kuna baadhi ya shule zenye vyoo vya kisasa kwenye shule za msingi na sekondari ambazo hazina huduma ya maji kutoka vyanzo vya uhakika.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mamlaka za Maji Vijijini na Mijini zimeelekezwa kuhakikisha kuwa taasisi za umma ikiwa ni pamoja na shule zinaunganishwa na mtandao wa maji katika maeneo yenye mtandao wa maji ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali ya kuhakikisha kuwa shule zinakuwa na vyoo vya kisasa vyenye huduma ya maji ni pamoja na ujenzi wa shule mpya unaojumuisha fedha za ujenzi wa miundombinu ya maji inayohusisha kuvuna maji ya mvua, kuunganisha na mifumo ya mamlaka za maji na kuchimba kisima, ujenzi wa miundombinu ya vyoo unajumuisha fedha ya ujenzi wa miundombinu ya maji tiririka na kutumia sehemu ya fedha ya ruzuku uendeshaji wa shule na kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa maelekezo hayo, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, Serikali haioni kwamba muda umefika wa kujiwekea *ultimatum* ya muda maalum kama miaka miwili au mitatu kuhakikisha kwamba shule zote za msingi na sekondari zina huduma ya maji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na kwamba huduma ya maji imepelekwa kwenye baadhi ya shule kumekuwa na changamoto ya ulipaji wa bili, matokeo yake baadhi ya shule zimekatiwa huduma ya maji kwa mfano Shule ya Msingi Kyombo imekatiwa huduma ya maji kwa sababu inadaiwa shilingi 400,000 tu.

Je, Serikali haioni kwamba kwa kutekeleza Sera ya Elimu Bila Malipo, kwa nini Serikali isiwe inalipa bili za maji ili wanafunzi wapate huduma za maji bure?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu maswali yake yote mawili kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweka kipaumbele kikubwa sana katika kuhakikisha kwamba shule zetu za msingi na sekondari zinakuwa na huduma ya maji ya uhakika na ndiyo maana tayari Serikali ilishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote kuhakikisha kwamba wanawasiliana na Mamlaka za Maji katika mikoa husika kupitia Katibu Tawala wa Mkoa ili kwenye zile shule ambazo hazina maji waweze kuchimba visima.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wote tunatambua Serikali imenunua mitambo ya kuchimba visima na imesambazwa katika mikoa yote 26. Kwa hiyo, tayari maelekezo yalitolewa na Serikali ili mitambo ile iweze kutumika katika kuhakikisha inachimba visima katika shule zetu, lakini pia Wakurugenzi watumie *channel* nyingine ya kuwasiliana na mamlaka za maji katika mikoa ili waweze kuunganisha maji katika sehemu ambazo zinatoa huduma za msingi ikiwemo katika shule zetu za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana pia na suala zima la ulipaji wa bili za maji; ni kweli kupitia fedha ile ya elimu bila malipo kuna fedha ya utawala ambayo pia inatumika katika kulipa bili za maji, lakini bili za umeme. Lakini ninaomba niendelee kusisitiza na kukumbusha Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kupitia Wakurugenzi wafahamu kwamba wajibu wa msingi wa kupanga maendeleo, kukusanya mapato na kugharamia huduma za msingi za kijamii ikiwemo katika sekta ya elimu, sekta ya afya; na kadhalika, ni wajibu wa msingi wa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo waendelee kubuni namna bora zaidi ya kuhakikisha kwamba wanagharamia gharama mbalimbali za kuhakikisha kwamba huduma za kijamii katika maeneo yao zinaimarika ikiiwemo pia katika upande huu wa sekta ya elimu. Kwa hiyo, kupitia Wakuu wa Shule, lakini kwa kushirikisha wazazi kwenye vikao vya wazazi wanakubaliana kimsingi ni namna gani gharama hizi wataweza kuzibeba, cha msingi ni watoto wetu wasikose huduma ya maji katika shule za msingi na sekondari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali kwa Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix Mbunge wa Buhigwe, sasa aulize swali lake.

Na. 564

**Kuchochea Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi Vijijini**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo kupitia utekelezaji wa mikakati ya huduma jumuishi za kifedha katika maeneo ya vijijini kwa kuhamasisha mabenki kufungua matawi kwenye maeneo ya vijijini, kukuza stadi za maisha na ujuzi miongoni mwa vijana kwa

kujenga na kuweka mazingira wezeshi ya ujenzi wa vyuo vya mafunzo ya amali ili kukuza ajira, kupitia upya mifumo ya uuzaji wa mazao ya kilimo, mifugo na misitu kwa lengo la kunufaisha wakulima, kurahisisha na kuwezesha mazingira ya kufanya biashara vijijini, kuweka mazingira maalum ya kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vijijini kwa lengo la kufanya ongezeko la awali la thamani *(primary processing)* katika sekta za kimkakati zikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi na misitu.

Mheshimiwa Spika, pia kuimarisha usalama wa chakula kwa kuboresha uhifadhi wa mazao, kuwapatia wakulima teknolojia za kisasa za uhifadhi wa chakula, kuendelea kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii kwa kuimarisha huduma za jamii, ikiwemo elimu, afya, maji, na umeme; na kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuvutia uwekezaji na maendeleo ya sekta binafsi kupitia kupitia programu za usambazaji wa umeme vijijini awamu ya tatu na ujenzi wa barabara za vijijini yaani *TARURA*, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ipi mikakati ya Serikali ya kujenga viwanda vijijini ili kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa vijijini na kuwatafutia masoko ya mazao hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, lini Serikali itapitia upya sera au kuleta toleo jipya la sera ya maendeleo vijijini ili ikidhi mahitaji ya maendeleo ya sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kavejuru kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mikakati mikubwa kuhakikisha kwamba tunakwenda kuongeza thamani ya mazao yetu tukumbuke kwamba sasa hivi tupo kwenye maandalizi ya dira ya mwaka 2050 ambapo Serikali imeweka mikakati mikubwa sana katika zile sekta ambazo tunaziona ni sekta ambazo zitakwenda kufufua uchumi wa nchi yetu na sekta hizo mojawapo ni sekta ya kilimo ambapo tumetambua kabisa kwamba katika sekta ya kilimo lazima tuongeze uzalishaji, lakini katika kipengele kingine lazima tuweke mazingira mazuri ya kuongeza thamani ya mazao yetu ili mazao yetu yawe na thamani, tunapokwenda kuyauza kwenye soko lolote lile aidha la ndani au soko la nje basi mazao hayo yaweze kuwa na thamani kubwa na hiyo iweze kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuzungumzia lile suala la sera ya maendeleo ndani ya hiyo hiyo *vision* ya mwaka 2050 tumekwenda kuimarisha na kwenda kuhakikisha kwamba tunakwenda kuweka mazingira mazuri ya maendeleo vijijini kama tulivyoanza sasa hivi tunapeleka umeme vijijini, tunapeleka barabara vijijini, tunapeleka mitambo ya simu kwa maana ya mawasiliano vijijini, hii yote ni kuweka mazingira mazuri ya kuhakikisha watu walioko vijijini wanafanya biashara vizuri na kuweza kuleta maendeleo katika maeneo yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, katika mipango ya muda mfupi na muda mrefu, je, Serikali imejipangaje kisera na kiutekelezaji kusaidia wafanyabiashara wadogo wadogo na wabunifu waliopo kule vijijini ili waweze kuongeza uchumi wao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba nijibu swali la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kusisitiza kwamba tunakwenda kumalizia sasa ile *vision* ya mwaka 2025 ambayo inaishia mwaka huu na mwakani tunakwenda kwenye mipango mipya ya dira ya mwaka 2050. Naomba nikuhakikishie tuna mipango mzuri sana ya muda mfupi na muda mrefu kuhakikisha kwamba tunawekeza kama Serikali kwenye zile sekta zote ambazo zinakwenda kuifufua uchumi wa nchi yetu na hizo itakwenda kusaidia wafanyabiashara wote wakubwa na wadogo ikiwemo wakulima kuwapa mazingira mazuri ya kufanya biashara na tutakwenda kufufua uchumi wetu mzuri zaidi kwa mwaka 2050 ambapo ndiyo *target* ya nchi yetu, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, bado Mheshimiwa Naibu Waziri anazungumzia *generally, specifically* mimi nataka kufahamu kwenye zao la korosho, kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba kuna mpango madhubuti kabisa wa kuhakikisha kwamba zao hili linakuwa ni zao linalotuletea pesa ya kutosha kabisa hasa ukizingatia limekuwa likionyesha hivyo sasa hivi kutakuwa na mpango gani kutoka kwenye Wizara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mchungahela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zao la korosho ni moja kati ya mazao Matano ya kimkakati ambayo nchi yetu au Serikali yetu imewawekea mkazo wa kipekee na kama nilivyotangulia kusema kwa mazao yote ya kilimo ikiwepo zao la korosho suala la kuzalisha kwa maana ya kuongeza *productivity* ndiyo jambo kubwa na la msingi ambalo Serikali imefanya uwekezaji wa hali ya juu; moja ni kuhakikisha kwamba tunatengeneza mifumo mizuri ya kuongeza uzalishaji wa mazao yote ikiwemo zao la korosho. Jambo la pili ni katika kuongeza thamani ya mazao, tukiweza kuweka uwezo wa nchi kuongeza thamani ya mazao katika mazao tunayozalisha ndipo tutapokwenda kuona tija ya mazao

yetu kwa maana tutayauza kwa bei juu na Serikali itaendelea kupata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa wakati uliopo tunaendelea kuhakikisha kwamba zao letu la korosho linaendelea kuuzwa kwenye yale masoko ambayo tunaona yanakuwa na tija kwa sababu zao letu la korosho limekuwa na bei ya kupanda na kushuka kutoka na soko la dunia, kwa hiyo ni lazima tutengeneze mazingira mazuri katika soko la ndani, kuongeza thamani na tuweze kuuza zao hilo kwa tija kubwa na tija hiyo iweze kwenda kwa wakulima, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali kwa Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 565

**Wawekezaji wa Biashara ya Carbon – Arusha**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani kuvutia wawekezaji wa biashara ya *carbon* katika Mkoa wa Arusha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Hamza majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni *(NCMC)* na kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatekeleza mikakati mbalimbali kuvutia wawekezaji wa biashara ya kaboni katika Mkoa wa Arusha. Mikakati hiyo ni pamoja na kuandaa kanuni za udhibiti na

usimamizi wa baishara ya kaboni za mwaka 2022 ambazo zimefanyiwa marekebisho ya mwaka 2023; kuanzishwa kisheria Kituo cha Taifa cha Kuratibu na Kufuatilia Biashara ya Kaboni *(National Carbon Monitoring Center- NCMC);* kutoa elimu kwa umma kuhusu biashara ya kaboni na kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua hizo, taasisi na kampuni mbalimbali zimeonesha nia ya kuwekeza kwenye biashara ya kaboni katika Mkoa wa Arusha hususani katika Halmashauri za Wilaya ya Karatu na Monduli. Taasisi na kampuni hizo ni pamoja na *The Nature Conservancy*, *Albrin*, *Soils for the Future Tanzania* na *Carbon Tanzania*.

Mheshimiwa Spika, biashara ya kaboni ni fursa adhimu ambayo ipo katika sekta nyingi. Hivyo, napenda kuwahamaisha sekta binafsi na wananchi wote kuendelea kuchangamkia fursa za uwekezaji katika biashara ya kaboni. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia sheria, kanuni miongozo na taratibu katika uendeshaji wa biashara hii ili wananchi wavutiwe na wanufaike na uwepo wa biashara hii, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa biashara hii ya *carbon* ni muhimu sana kwa ajili ya kutuongezea mapato kwenye halmashauri zetu; ni upi makakati wa Serikali kushirikiana na sekta binafsi kutafuta masoko ya uhakika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili uelewa wa biashara hii ya hewaukaa bado ni mdogo sana hususani kwenye jamii za kifugaji ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha wananchi wanapatiwa elimu juu ya faida ya biashara hii? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu masuala mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zaytuni kama ifuatavyo; lakini nichukue

fursa hii nimpongeze sana kwa kuwa amekuwa na hamasa kubwa ya kutaka kujua faida ya fursa na elimu ya biashara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze tu na suala hili la masoko kwa wadau mbalimbali, nakumbuka mwezi wa nne mwaka huu tulifanya mkutano mkubwa katika Mkoa wa Dar es Salaam na mkutano ule ulikuwa unahusisha masuala haya ya baishara ya *carbon* na tuliweza kuwaalika watu mbalimbali wakiwemo wawekezaji, taasisi za Serikali, taasisi binafsi, viongozi wa Serikali kwa maana kwamba Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, ma-*DAS* na ma-*RAS* wote ikiwa na lengo kwanza kuwapatia elimu, lakini pili ilikuwa ni kueleza fursa zinazopatikana kutokana na biashara hii, lakini kubwa zaidi ilikuwa ni kuwaonyesha wapi masoko yanapatikana katika biashara hii.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu kwamba Serikali itaendelea kuendelea kutafuta masoko ya biashara hii, wawekezaji waje na tayari wapo wawekezaji ambao wameshajitokeza kwa ajili ya kuanza kuufunga mkataba na kufanya biashara na Serikali ili kunufaisha wananchi. Tumetoa elimu, tumeanza na makundi mbalimbali yakiwemo ya wafugaji, wakulima, watendaji wa Serikali na viongozi mbalimbali tumekuwa tukiwapa elimu, lakini nimwambie tu Mheshimiwa kwamba kwa sababu elimu hii bado haijaenea nchi nzima tutaedelea kutoa elimu kwenye makundi tofauti hasa kwa makundi ya wafugaji hasa na wakulima hasa wale wa vijijini kwa sababu wao ndiyo ambao wanasimamia misitu mikubwa inayozalisha hii *carbon,* nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul Maalim swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, kuna mkakati gani wa kuwashirikisha wadau wa Zanzibar ili kunufaika na biashara hii ya hewa ukaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuona kwamba kuna

misitu mikubwa Zanzibar tena ni ya asili na miti mikubwa ambayo ina uwezo wa kuzalisha na kutoa *carbon* nyingi kwa sababu ipo muda mrefu tumeona na wenzetu Zanzibar tushirikiane nao, tumeshirikiana na *ZEMA*, tumeshirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi, wa Waheshimiwa Masheha, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri ili lengo na madhumini kupeleka elimu hii na kwa sababu fursa hii ipo Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nimwambie Mheshimiwa Abdul kwamba kutokana na elimu tuliyoitoa sasa Zanzibar inakwenda kunufaika na biashara hii ya hewa ukaa, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba kuuliza pale Moshi Mjini kuna Msitu wa Rau ambao upo chini ya *TFS,* je, Wizara ipo tayari kuja tukupa mafunzo manispaa na *TFS* namna ambavyo tunaweza kushirikiana kwenye hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Priscus Tarimo swali lake kwamba Wizara tuko tayari na kwa sababu tumeshaanza mikoa mingi sana kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI tutahakikisha kwamba tunafika hapo na tutaanza kutoa maelekezo leo hii ili kazi hii ya kuelimisha na kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na hewa hii ama biashara ya hewa ukaa ianze kufanya kazi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali kwa Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 566

**Mikopo kwa Wanawake wa Vijijini**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali inafanya jitihada gani kuhakikisha mikopo ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inawafikia wanawake wa vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake wa Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na taasisi za fedha inatumia vyombo vya habari, maafisa maendeleo ya jamii, maafisa biashara walioko kwenye halmashauri zote nchini, maafisa mikopo wa benki, viongozi wa wafanyabiashara ndogo ndogo pamoja na viongozi wa Serikali katika ngazi mbalimbali kufanya uhamasishaji na kutoa elimu kuhusu mikopo inayotolewa na Serikali ili wanawake na makundi mengine waendelee kujitokeza kupata mikopo hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa waombaji wa mikopo ya wanawake ni wengi kuliko fedha zinazotolewa Serikalini; je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wigo wa mikopo hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali imefanikiwa kuzifikia halmashauri ngapi ikiwa ni mkakati wa kutoa elimu kwa wanawake vijijini juu ya uwepo wa fursa ya mikopo nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Maryam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Maryam kwa kufuatilia mikopo ya wafanyabiashara ndogo ndogo hasa kina mama.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza Serikali inaendelea kuimarisha utoaji wa mikopo wa 10% na Serikali inaendelea kuhamasisha kupitia Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii kutpoa mikopo ile ya 10% kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI lakini Wizara yenyewe ya Maendeleo ya Jamii sasa imeshirikiana na taasisi za benki za NMB kutoa mikopo ya wafanyabiashara ndogondogo ili kujiwezesha kiuchumi na kuhakikisha kwamba wananchi wanendelea vizuri na mikopo hii na kupata fursa hasa katika vijiji vyetu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili; Serikali tumefanikiwa kuzifikia halmashauri zote 184 kutoa elimu na kupata fursa kwa wananchi hawa vijijini ili Mheshimiwa Rais nia yake na madhumuni yake ya kuwawezesha wanawake hasa wanawake wenye biashara ndogo ndogo waweze kufaidika na Serikali yao ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kuishukuru Wizara kadri mnavyopambana na kuboresha maeneo haya 10% lakini swali langu la msingi; Mheshimiwa Waziri upo tayari kwenda

Mbogwe nina vijiji 87, nina watu wenye ulemavu wanaohitaji mikopo hii ili ukatoe elimu waweze kukuelewa vizuri?

**SPIKA:** Najaribu kutafakari Mheshimiwa Waziri mwenyewe atakuwa *busy* anawaza kwenda kwenye fomu baada ya Bunge hili sasa ataenda lini na leo ni tarehe 11 tayari.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, hata siku moja tu ya *weekend* mimi naweza nikambeba tukaenda ili wapate elimu vizuri wananchi wangu. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Kwa kweli, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge nipo tayari kufatana naye kwa vile mimi ni mama na ambaye ninatoa elimu na nahitaji wanawake wote waweze kujiwezesha basi nipo tayari kufatana naye kuwapa elimu wananchi wa mkoa wake, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali kwa Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 567

**Hitaji la Miradi ya Maji – Mbinga**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kujenga miradi ya maji katika Kata za Kikolo na Kilimani na Vijiji vya Mtama, Tukuzi, Masimeli, Lupilo, Miembeni na Mateka – Mbinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Kundo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imekamilisha utekelezaji wa mradi wa maji Mkwaya uliopo Kata ya Kilimani Wilaya ya Mbinga. Kupitia programu maalum ya uchimbaji wa visima 900, Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu rahisi ya kutolea huduma *(point source)* katika vijiji vitano ikiwemo Vijiji vya Kikolo na Nzopai vilivyopo Kata za Kikolo na Kilimani. Aidha, Serikali inaendelea na upanuzi wa Skimu ya Maji ya Kijiji cha Tanga kwa ajili kufikisha huduma ya maji kwenye Vijiji vya Kata ya Mateka ambapo utekelezaji wake umefikia 60% na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2025.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali ipo kwenye hatua za ununuzi wa kuwapata wakandarasi wa kutekeleza miradi ya maji katika Vijiji vya Mtama na Tukuzi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi ya maji kwa ajili ya kunufaisha Vijiji vya Masimeli, Lupilo na Miembeni ambapo usanifu wake umekamilika.

**SPIKA :** Mheshimiwa Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini pia naipongeza Serikali kwa kuendelea kutatua changamoto zinazojitokeza za maji katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kijiji za Nzopai kipo katika Kata ya Kilimani lakini umbali kutoka Kilimani mpaka Nzupai ni zaidi ya kilometa 10 na katika Kijiji cha Nzopai imejengwa *point source;* sasa nilitaka nijue ni lini Serikali itajenga miundombinu rahisi *point source* katika kijiji cha Kilimani? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nashukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuipongeza

Serikali kwa kuendelea kutatua changamoto za maji kwa wananchi wake na sisi tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutufanyia wepesi sisi Wizara ya Maji kuendelea kuchukua hatua kulingana na fedha ambazo anaendelea kuzitoa.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kuwa Kijiji cha Nzopai ni kweli kabisa kina umbali wa kilometa karibia kumi lakini tayari tumeshaanza usanifu wa kuona namna gani tunawapelekea maji katika hilo eneo, lakini eneo la Kilimani ni pana kidogo ambapo tutazingatia mahitaji ya wananchi kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE.OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Miradi ya Maji ya Chani, Kalugera, Bisheke na Nyakasimbi Jimbo la Karagwe, ni lini wakandarasi watalipwa ili kumtua mwanamke ndoo kichwani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Oliver, mradi huu wa Chani ninaufahamu na ulikuwa una changamoto kwa sababu ulipata wakandarasi wawili na baadaye mkandarasi mmoja akashindwa kukamilisha mradi huu na baadaye tukampatia mkandarasi anaitwa *Otonde Construction* na sasa ameshaingia *site* na jana tumewasiliana na *RM* Mkoa wa Kagera tayari wamepokea shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kumlipa mkandarasi ili aendelee kuhakikisha kwamba Mradi wa Chani - Kalugera uweze kukamilika na wananchi wa eneo hilo wapate huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Kampuni ya *Mponela Construction* imeanza kutekeleza Mradi wa Ndoleleji hadi Masanga tangu mwezi Machi,

2023 na ulipaswa kukamilishwa mradi huu mwezi Machi, 2024; je, Serikali inatoa kauli gani kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa kwa haraka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Butondo kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya kwa wananchi wake wa Kishapu, lakini pia mradi huu wa Ndoleleji-Masanga ni mradi ambao kweli unatekelezwa na *Mponela Construction* na sasa umefikia 80% ya utekelezaji wake. Kwa hiyo, niwaombe *RM* Mkoa wa Shinyanga ahakikishe kwamba mradi huu unakamilika kwa kadri ambavyo unatakiwa ili wananchi wapate huduma ya maji safi na salama, lakini pia na sisi Wizara tutahakikisha kwamba tunaufuatilia kwa ukaribu sana kuona kwamba unakamilika kadri ya ambavyo unatakiwa, ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yaulizwe kwa kifupi na Wabunge mnaozungumza na simu Bungeni Kanuni zinakataza. Mheshimiwa Ally Makoa, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kupata *commitment* ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na mradi mkubwa wa pale Kondoa Mjini ambao umesimama kwa muda mrefu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, mradi ule wa Kondoa Mjini ni kweli kabisa kwamba kulikuwa na changamoto ya madai kwa wakandarasi na sasa tayari tumeshakaa na wakandarasi, lakini pia tunaendelea kukaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili kuwezesha mkandarasi huyo arudi *site* na tayari Wizara ya Fedha wametuomba tupeleke madai hayo ili kuhakikisha kwamba mkandarasi huyo analipwa ili aweze kuendelea na utekelezaji wa mradi huo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Serikali iliahidi kukamilisha au kuanza kujenga mradi wa maji kutoka Ziwa Tanganyika kuyaleta Makao Makuu ya Mkoa wa Katavi; je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa mradi huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshaanza utekelezaji wa mradi huo wa kuhakikisha kwamba tunatumia maji ya kutoka Ziwa Tanganyika kwa ajili ya Mkoa wa Katavi, lakini ukiwemo Mkoa wa Rukwa pamoja na Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, ninamuomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na subira wakati *feasibility study* inakamilika, *details design* ili tuweze kujua ni gharama itahitajika na Serikali iweze kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini mradi wa maji ambao uko kwenye Kata ya Kinyala Wilaya ya Rungwe unaotegemewa sana na vijiji vinne, Vijiji vya Igembe, Rubigi, Kipande na Isumba utakamilika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa swali hili, lakini pia ni kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Rungwe, lakini pia naomba nilipokee kwa ajili ya kutoa taarifa sahihi kwa

ajili ya kujua kwamba umefikia hatua gani kwa sababu mpaka sasa sina *statistics* kamili, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Kata za Mbondo na Kilimarondo hakuna maji safi na salama na maeneo haya yana vituo vya afya ambavyo navyo vinahitaji maji na tayari tumepeleka maombi ya shilingi milioni 250 kwa ajili ya kupeleka maji kwenye maeneo haya.

Ni lini Serikali itaupatia hizo fedha kwa ajili ya kupeleka maji safi na salama kwenye maeneo haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, vituo vya afya kwa ujumla wake taasisi za umma, vituo vya afya, shule, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inatoa kipaumbele kuhakikisha kwamba wananchi hao au wanafunzi katika shule wanapata huduma ya maji safi na salama ili kuepusha magonjwa ya mlipuko.

Mheshimiwa Spika, maombi hayo kama ameshayaleta tunaenda kuyatazama na kuhakikisha kwamba tunayatekeleza kwa haraka zaidi, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Bunda Mjini lina miradi tisa ya maji ambayo inahitaji shilingi bilioni 14 kwenye kata mbalimbali ikiwepo Wariku, Bunda Mjini ambapo mradi unatoka Mlima Bomani kwenda Nyiendo na maeneo mengine. Ni lini sasa mtatoa hizo pesa ili wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini wapate maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninamshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya na pia kwa kuendelea kutukumbusha na kutushauri pale panapowezekana na sisi Serikali kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Serikali sikivu ambayo inachukua maoni ya kila mtu lengo ni kwamba tunaboresha na kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Serikali iko tayari na itatoa fedha na maeneo hayo yatapata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

Na. 568

**Kuanza kwa Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Maji Namtumbo**

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Je, lini mradi mpya wa kuboresha upatikanaji wa maji Namtumbo utaanza kama ulivyoombwa kwa Mheshimiwa Rais alipotembelea Namtumbo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba na mkandarasi kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Namtumbo. Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa madakio mawili *(intakes)*, ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 1,000,000, ulazaji wa mabomba umbali wa

kilometa 30 sanjari na ufungaji wa dira za malipo ya kabla *(pre-paid water meter)* kwa wateja 50. Mradi huo utatekelezwa kwa muda wa miezi 12 ambapo kukamilika kwake kutaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka 57% ya sasa na kufikia 95% ya watu waishio kwenye Mji wa Namtumbo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Serikali ina mpango gani mkakati wa kuhakikisha kwamba Watanzania ambao hawana *source* ya maji kutoka kwenye maziwa wanapatiwa maji safi na salama?

Swali la pili, shule zetu na taasisi za afya nyingi hazina visima au maji na bado hawapo katika mpango huo wa kupelekewa maji, sasa katika kuhakikisha kwamba wanawapatia maji safi na salama Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inachimba visima kwenye hizi taasisi ambazo nimezitaja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninamshukuru Mheshimiwa Esther kwa maswali mazuri.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya maji, tuna vyanzo vya aina mbalimbali, maji juu ya ardhi, maji chini ya ardhi, lakini pia na *man made* maji, maana yake kwamba tunatengeneza mabwawa ili kuhakikisha kwamba kuna maeneo ambayo kuna ukame, lakini tunaweza tukateka yale maji ya mvua, tukayakusanya na yakaweza kutumika kama chanzo.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo kuna maziwa watatumia maziwa, mito na kadhalika, pale ambapo kuna maji chini ya ardhi tutatumia maji chini ya ardhi kwa kuchimba visima. Pale ambapo chini ya ardhi hakuna maji na hakuna vyanzo vingine tutajenga mabwawa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwenye taasisi za Serikali kama ambavyo nimejibu hapo kabla, taasisi za Serikali kuna maeneo ambayo maji yanapatikana chini ya ardhi tutachimba visima katika vituo vya afya, shule na kadhalika, lakini kama hakuna chini ya ardhi maana yake hatutachimba visima isipokuwa tutatumia miradi iliyokaribu na maeneo ya taasisi za umma ili kuhakikisha kwamba tunawafikishia mtandao ili waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuzingatia maeneo yote ya Watanzania ambao wanahitaji huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga sasa aulize swali lake.

Na. 569

**Ujenzi wa Mahakama Tarafa ya Kiponzelo – Kalenga**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mahakama Tarafa ya Kiponzelo – Kalenga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Jumanne Sagini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania imeendelea kutekeleza Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama wa mwaka 2021/2022 - 2025/2026. Majengo hayo yanajengwa na kukarabatiwa kwa awamu kwa kuzingatia mpango huo kadri fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango huo unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026 ambapo kwa sasa hatua za kuuhuisha mpango huo zinaendelea. Aidha, majengo ya Mahakama ya Mwanzo Kiponzelo yatajumuishwa katika mpango huo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Tarafa ya Kiponzelo kutokana na ushirikiano wao na Mahakama kwa kufanya ukarabati wa jengo lililopo sasa, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza niishukuru Serikali kwa kuiweka Mahakama hii kwenye mpango, lakini pia nimshukuru Afisa Tarafa wa Tarafa ile Rukia Hassan kwa kuanza kuhamasisha wananchi waanze ukarabati. Mahakama ile ni moja ya Mahakama kongwe zilizojengwa mwaka 1939 na kukabidhiwa kwa familia ya Chifu na Hakimu wa Kwanza alikuwa Mussa Adam Sapi Mkwawa.

Je, haioni sasa kwa sababu ya umuhimu wa kihistoria tukaipa kipaumbele tukaanza kujenga sasa ili irudishe historia, lakini isaidie wananchi wengi zaidi ya vijiji 15 watatumia pale? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa uzito wa historia aliyozungumza Mheshimiwa Kiswaga naomba nimuahidi kwa kumhakikishia kwamba kama nilivyoeleza mpango huu tunaouhuisha Mahakama hiyo itapewa kipaumbele na kwa vile unaanza tu mwaka kesho asiwe na mashaka, utekelezaji utaanza na sisi wa Katiba na Sheria tutakwenda kushuhudia ukarabati ukifanyika wa kiwango cha kuridhisha, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaishukuru Serikali kwa ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mbulu, hivi sasa ujenzi umesimama kwa zaidi ya miezi sita; je, ni lini Serikali itarudi kuja kujenga ule ujenzi wa Mahakama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Zacharia, Mbunge wa Mbulu kwamba Serikali kupitia Idara ya Mahakama na hususan Mtendaji Mkuu wa Mahakama atahakikisha kwamba mpango uliopitishwa na ujenzi umeanza hakuna Mahakama inayosimama. Najua palikuwa na changamoto ya kufanya mapitio ya utekelezaji wa mpango huo na kadri mapitio hayo yatakavyokamilika *then* wakandarasi watarudi *site* kuhakikisha kwamba Mahakama ya Wilaya ya Mbulu inakamilishwa kama ilivyopangwa, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza Wizara; ni lini watahamisha Mahakama ya Mwanzo katika eneo la Kituo cha Afya Sangabuye na kwenda kwenye eneo ambalo wameshapewa la hekari tano ili kupisha upanuzi wa kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Angeline Mabula, Mbunge wa Ilemela kwa namna anavyofuatilia ujenzi wa mahakama hii na kwamba kuweka mahakama eneo la kituo cha afya kwa kweli ni malengo yanayosigana na kwa maana hiyo naomba nimpe uhakikisho, tumeshazungmuza na Mtendaji Mkuu wa Mahakama, hivi karibuni atatuma wataalam wake waende wa-*assess* hili eneo la hekari tano lililokwishatolewa ili tunapoingia kwenye mpango wa pili wa utekelezaji wa mkakati wa kuiboresha sekta ya mahakama basi Mahakama inayoitajwa Sangabuye inapewa kipaumbele, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni Mbunge wa Chemba sasa aulize swali lake.

Na. 570

**Ujenzi wa Barabara ya Zamahero – Donsee na Goima Bicha**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza: -

Je, lini Barabara za Zamahero – Donse na Goima - Bicha zitajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ipo katika hatua ya maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Goima – Bicha yenye urefu wa kilometa 35.36. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hiyo imepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa upande wa barabara ya Zamahero – Donsee kilometa 45.36, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Usanifu utakapokamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara hizo ni *interchange* ya barabara kuu ya kutoka Kibarashi - Mrijo - Chemba hadi Singida. Sasa nataka kujua ni lini sasa barabara kuu hii itajengwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, hii barabara kuu ya Kibarashi - Chemba kwenda Kwa Mtoro ni barabara ambayo sasa tumeanza kuijenga kwa awamu, na tutaanzia upande wa pale tulipoishia kilometa 50 kutokea Handeni na tutaendelea kuijenga kwa kiwango cha lami ambapo tumeipangia fedha katika mwaka ujao wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari kuharakisha usanifu wa kina na upembuzi yakinifu wa Barabara ya Nangwe - Kisamba na Kondoa ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tuko tayari na ndiyo maana tumeipanga katika mpango ili kurahisisha mawasiliano ya kati ya Wilaya ya Hanang na Kondoa kwa maana ya Manyara na Mkoa wa Dodoma kupitia Kondoa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero sasa aulize swali lake.

Na. 571

**Barabara ya Kuunganisha Mkoa wa Morogoro, Njombe, Lindi na Ruvuma**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuunganisha Mkoa wa Morogoro, Njombe, Lindi na Ruvuma kwa barabara ya lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza ujenzi wa sehemu ya Ifakara – Mbingu (kilometa 62.5) na Mbingu – Chita (kilometa 37.5) ambapo sehemu iliyobaki ni ya kuanzia Chita hadi mpakani mwa Morogoro na Njombe. Kwa upande wa barabara ya kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Ruvuma, Serikali imesaini Mkataba wa Ujenzi wa sehemu ya barabara hiyo kwa utaratibu wa sanifu na jenga kuanzia Ifakara – Lupiro – Mtimbira (kilometa 112). Kwa upande wa kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Lindi kwa barabara ya Nachingwea – Liwale – Ilonga – Mwaya hadi Mahenge, taratibu za manunuzi ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii zinaendelea, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kupata hizo barabara zetu tatu ya Ifakara - Kidatu na mkandarasi wa Ifakara - Mlimba nimeona ameanza.

Swali langu la kwanza, je, hii barabara ya Ifakara – Mbasa - Lipangalala kwenda Malinyi mkandarasi ataanza lini?

Swali la pili, katika Barabara ya Ifakara - Kidatu bado kuna wananchi wanadai fidia pamoja na hii Barabara ya Ifakara - Kikwawila itapita Mbasa - Lipangalala hawajalipwa fidia. Je, ni lini wananchi hawa watalipwa fidia yao? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, hii barabara ya kutoka Ifakara - Lupiro - Mtimbira kwenda Malinyi kama nilivyosema kwenye jibu la msingi tumeshasaini na

mkandarasi sasa hivi anasubiri tumlipe ameshaleta maombi yake ya fedha ya awali ili aweze kuanza kazi na mara atakapokuwa amelipwa basi taanza hiyo kazi kuzijenga hizo kilometa 112.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watu ambao bado hawajalipwa na wale ambao watatakiwa kulipwa kupisha hii barabara ya ujenzi, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tulishafanya tathmini na wale ambao walikuwa kwa bahati mbaya hawakulipwa kati ya Ifakara na Kidatu madai yao tulishayapokea na yanafanyiwa kazi Hazina ili waweze kulipwa fedha zao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 572

**Barabara ya *Ring Road* Kuanza Kutumika**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya *ring road* itaanza kufanya kazi ili kuzuia msongamano uliopo Barabara ya Morogoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara ya mzunguko wa nje katika Jiji la Dodoma ni barabara ambayo ina urefu wa kilometa 112.3. Dhumuni kubwa la ujenzi wa barabara hii ni kupunguza msongamano wa magari yakiwemo malori kutokupita katikati ya Jiji la Dodoma. Ujenzi wa barabara yote umefikia 83% na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 31 Agosti, 2025, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia naona umeketi. Samahani Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri

nakubaliana na majibu yake ambayo ni mazuri kutokana na Serikali, lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Mheshimiwa Waziri unaweza kulithibitia Bunge hili kwamba tarehe hiyo uliyoitaja kwamba hiyo njia itakuwa tayari? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kama ulivyozungumza kwamba kuna msongamano wa magari kutoka hii njia ya Morogoro, kwa mfano kuna magari ya mizigo, mabasi makubwa ya abiria, gari za watu binafsi, bodaboda na daladala yote yanapita njia hiyo, hata useme utatoka mapema nyumbani ili uwahi kazini ujue utachelewa tu.

Je, mnaweza mkatusaidia kwa kutujengea barabara nne ili ziweze kupata kupita gari hizo kwa ufasaha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya Mbunge kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Spika, wale ambao wanapata bahati ya kuangalia kinachoendelea, kazi iliyofanyika ni kubwa sana na tuna *lot* mbili; *lot* moja ya kwanza tunategemea pengine itakamilika hata kabla ya tarehe hii na *lot* ya pili ndiyo tunategemea ikamilike tarehe 31 Agosti kwa hizo kilometa 112 na wakandarasi wametuhakikishia kwamba watahakikisha kwamba wanakamilisha na hasa kuhakikisha kwamba ile barabara yote inapitika na lengo ni kwamba hata kama itakuwa bado pengine alama, lakini malori yanayotoka Dar es Salaam ama Mwanza kwenda Singida yaanze kupita kuanzia Mtumba kwenda huko na kwenda Nala bila kupita hapa na kwa sasa kwa maana ya njia za kutembelea ni karibu zimekamilika barabara yote kuanzia mtumba mpaka Nala huko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutengeneza hizi njia hapa katikati nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wakazi wa Dodoma, lakini na Watanzania kwa ujumla kuwa

tunachokwenda kufanya sasa hivi kuanzia kwenye *keep left* hii hapa tutajenga njia nne kutoka hapa mpaka *CBE* na kutoka *CBE* mpaka Mtumba zitakuwa njia sita na kutoka Mtumba kwenda Chamwino zitakuwa ni njia nne. Halikadhalika kutoka *keep left* ya Bahi kwenda *ring road* ya huku, lakini kutoka pia *keep left* ya Bahi kwenda Mkonze zitakuwa ni njia nne.

Kwa hiyo, taratibu zinaendelea na muda si mrefu ujenzi utaanza tukisaidiana na wenzetu wa *World Bank,* lakini pamoja na hiyo njia ya mzunguko wa nje tuna mzunguko wa kati na mzunguko wa ndani ambao tayari usanifu unaendelea kwa kusaidiana na wenzetu wa *JICA,* ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa George Mwenisongole.

Na. 573

**Kuchimba Madini ya Dhahabu Vijiji vya Idiwili, Iyula B na Idunda – Vwawa**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE K.n.y. MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kuchimba madini ya dhahabu kwenye Vijiji vya Idiwili, Iyula B na Idunda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Idiwili, Iyula B na Idunda vilivyoko katika Jimbo la Vwawa, Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe vina

viashiria vya uwepo wa madini ya aina mbalimbali ikiwemo dhahabu, shaba na madini adimu *(rare earth elements)*.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili Serikali kupitia Wizara ya Madini imetoa leseni nane za uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu *(PMLs)* na utafiti wa uchimbaji mdogo unaendelea katika leseni hizo husika. Pia kuna maombi 20 ya leseni ndogo za uchimbaji madini ya dhahabu na mchakato wa kutolewa leseni hizo unaendelea. Aidha, katika eneo hilo kuna leseni mbili za utafiti wa madini ya shaba na maombi mawili ya leseni za utafiti wa madini ya shaba, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; katika hizo leseni ambazo Serikali imetoa ni zipi *specific* ni kwa ajili ya Kijiji cha Idiwili, Idunda na Iyula B?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwenye Kata ya Bara na Kata ya Magamba katika Jimbo la Mbozi kuna watu wamehodhi leseni za uchimbaji kwa muda mrefu na hawazifanyii utafiti wala kunini. Nini mpango wa Serikali wa kuzichukua hizi leseni ili zitumike kwa watu ambao wenye nia ya dhati ya kufanya utafiti na kuchimba madini kwenye kata hizo? Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa George Mwenisongole aliyeuliza haya maswali ya nyongeza na swali la msingi kwa niaba ya Mbunge mhusika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *specifically* kwamba ni vijiji gani vina leseni gani zinazoendelea kuendelezwa kwa uchimbaji mdogo pamoja na utafiti sitakuwa na jibu lake hapa

mezani lakini naomba baada ya kutoka hapa wataalam wetu walioko kule katika Mkoa wa Kimadini wa Songwe na Mbeya wanaweza kutusaidia kupata majibu ya mtawanyiko wa hizo leseni ndogo za eneo la utafiti.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili kuhusu Bara na Magamba kule Mbozi watu waliohodhi leseni kwa mujibu wa Sheria ya Madini, Sura Namba 123 tuna utaratibu kwamba mtu aliyepewa leseni ya utafiti asipoweza kutoa taarifa za kila robo mwaka kwa Serikali kupitia taasisi yetu ya Jiolojia na Utafiti *(GST)* anapewa hati ya makosa na asipoweza kujirekebisha leseni hiyo hufutwa na kuwa wazi kwa ajili ya mwombaji mwingine ambaye yuko tayari kufanyia utafiti na hili lina-*apply* pia kwa wanaopewa leseni za uchimbaji. Asipoweza kuendeleza leseni yake iwe ndogo au iwe kubwa ndani ya miezi 18 tangu apewe ile leseni atapewa hati ya makosa na asipoweza kuijibia basi leseni hiyo itafutwa na ndiyo maana zaidi ya leseni 2600 mpaka sasa zimeshafutwa kwa muktadha huo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 574

**Mashindano ya *AFCON* Mwaka 2027**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa Serikali kuandaa timu ya Taifa madhubuti itakayowakilisha Taifa katika mashindano ya *AFCON 2027* tukiwa kama wenyeji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)* imeweka mikakati ya muda mfupi, wa kati na ya muda mrefu kwa ajili ya maandalizi ya timu ya Taifa. Mikakati hiyo inajumuisha:-

(i) Kuimarisha ligi ya ndani kwa kuhakikisha ushindani na nidhamu ya michezo ili kuibua vipaji bora vya wachezaji wa ndani;

(ii) Serikali kwa kushirikiana na *TFF* imeanda programu za kusimamia na kulea timu za Taifa za vijana walio chini ya miaka 15, 17 na walio chini ya miaka 23 ili kuandaa timu ya Taifa ya wakubwa iliyo imara na madhubuti itakayoleta ushindani katika mashindano ya *AFCON 2027;*

(iii) Serikali kwa kushirikiana na *TFF* itaendelea na mpango wa kufanya *scouting* kwa wachezaji wa *diaspora* katika mataifa mbalimbali duniani ambapo hadi sasa mpango huu umeonesha matokeo chanya kwa kujumuisha wachezaji hao kwenye mechi ambazo timu ya Taifa *(Taifa Stars)* ilifanya vizuri na kufanikiwa kufuzu kushiriki mashindano ya *AFCON*; na

(iv) Kuboresha program mbalimbali za huduma kwa timu hizi ikiwa ni pamoja na kuboresha benchi la ufundi, programu za lishe na kuzipatia vifaa mbalimbali vya michezo kulingana na mahitaji, pomoja na kuongeza motisha kwa timu yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa uweyeji wa *AFCON* ni heshima kubwa na fursa ya kihistoria, hivyo, tumejipanga kuhakikisha timu yetu haishiriki tu, bali inashindana kwa kiwango cha juu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zidadu Hassan Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kuna viwanja vya mashindano na maeneo ya michezo ambayo yapo katika halmashauri zetu zote nchini ambapo maeneo hayo yanasaidia kuibulia vipaji vya michezo mbalimbali. Kuna baadhi ya halmashauri ambazo yanabadilisha matumizi ya maeneo yale na kuyauza ili kuongeza ama kupata mapato ya ndani.

Je, Serikali imejipangaje kuzuia hilo ili kuyalinda maeneo hayo yaendelee kuibulia vipaji vya michezo mbalimbali kwa vijana wetu wa sasa na vizazi vijavyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali imejipangaje kuimarisha ligi za ndani kama msingi wa timu ya Taifa ili kuwa na timu ya Taifa bora ambayo kuelekea *AFCON 2027* ili kupata timu ya Taifa bora ambayo itashindana na siyo kushiriki? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini kwa ufuatiliaji mzuri wa shughuli za wapiga kura wake ikiwemo shughuli za michezo na naamini Wana-Tunduru Kaskazini wanaliona hili na hawata kuangusha muda utakapowadia.

Mheshimiwa Spika, kwenye kujibu maswali yake; swali la kwanza ni kuhusiana na kuvamiwa kwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za michezo. Kweli nakiri kumekuwa na jambo hili likitokea mara kwa mara na mimi binafsi nimekuwa nikiingilia maeneo mbalimbali ambayo yalikuwa na migogoro ya aina hii ambapo maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za michezo yamekuwa yakibadilishiwa matumizi na kutumika kwa ajili ya mambo mengine. Kwa mfano mgogoro ulliotokea kwenye

Halmashauri ya Korogwe na ili kuondoa jambo hili moja kwa moja suluhisho la kudumu ambalo tulilifikiria ni kuanzishwa kwa mamlaka ya usimamizi wa viwanja vya michezo nchi nzima ambapo mamlaka hii sasa tuko katika hatua za mwisho za kuianzisha na ambapo jukumu lake la kimsingi litakuwa kwanza kuhakikisha maeneo haya hayavamiwi, lakini kuboresha na kusimamia maeneo mbalimbali ambayo yanatakiwa kutumika kwenye shughuli za michezo.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kungu ya kwamba mamlaka hii ipo katika hatua za mwisho za uanzishwaji wake na shughuli yake ya msingi miongoni mwa ambazo itakuwa ikizifanya itakuwa ni hii.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili la kuimarisha ligi za ndani, hata wakati najibu swali lake la msingi mipango mingi ambayo Serikali inaifanya kwa kushirikiana na *TFF* lengo lake hasa ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha ligi za ndani ili kuwa na timu bora za Taifa. Mipango kama kuimarisha timu za ndani za vijana chini ya miaka 15, 17 na 23, lakini hali kadhalika ujenzi wa miundombinu bora ya michezo yeye atakuwa ni shahidi kwa sababu tuko naye kwenye Kamati na nafahamu jinsi Serikali inavyowekeza, lengo likiwa kuwekeza miundombinu bora ya kitaifa lakini kuwekeza miundombinu bora ya mikoani na kuhakikisha tunafika mpaka kwenye halmashauri ili vijana wetu wapate maeneo mbalimbali ya kufanya shughuli zao za michezo lakini pia na programu mbalimbali za kuwajengea uwezo walimu, waamuzi wa ndani na wachezaji na kuimarisha uwezo wao wa kufundisha, kucheza na pia weledi wakati wa kufanya shughuli zao. Yote inalenga katika kuhakikisha tunaimarisha ligi za ndani na hatimaye kuimarisha timu yetu ya Taifa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, moja kwa moja kwenye swali.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kuimarisha timu ya Taifa ni pamoja na kuhakikisha kwamba sheria na taratibu za michezo zinafuatwa nchini. Ligi yetu inaelekea

mwisho, lakini kumekuwa na mvutano wa hizi timu mbili na viongozi wa *TFF*. Ipi kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, unataka kumsaidia kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kama ambavyo unafahamu shughuli za mchezo wa mpira wa miguu zina mamlaka zake za kimataifa na za kitaifa na tumekuwa tukisisitizwa mara kwa mara Serikali kutokuingilia moja kwa moja uendeshaji wa shughuli hizo ili kuepuka kuja pengine hata kufungiwa na *FIFA* katika nyakati hizi ambapo kitakwimu nchi yetu inafanya vizuri sana katika uendeshaji wa shughuli za mpira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, mamlaka za uendeshaji na usimamizi wa shughuli za mpira wa miguu nchi hii ni *TFF* ambalo ni Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini, lakini pia na Bodi ya Ligi Kuu ambazo Serikali hata taarifa ambazo tunazitoa hapa tuna-*rely* kwenye taarifa tunazopata kutoka kwao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchezo anaousema tunafuatilia kwa ukaribu jinsi ambavyo mgogoro huu unaendelea kutatuliwa huku tukijaribu kwa kiwango kikubwa kabisa kutoingilia moja kwa moja maamuzi ya *TFF* na Bodi ya Ligi, lakini tumekuwa tukifuatilia kwa ukaribu *eyes on, hands off* huku tukisisitiza *TFF* na Bodi ya Ligi kufuata na kutekeleza kanuni na sheria ambazo wamejiwekea za uendeshaji wa mpira wa miguu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kifupi kabisa ni kwamba tunafuatilia jambo hili lakini tukihakikisha kwamba hatuingilii moja kwa moja na kupelekea nchi yetu kufungiwa kwa vile mchezo wa mpira wa miguu unajiendesha wenyewe, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante. Mheshimiwa Ester Bulaya hebu sema unayosema kwenye kisemeo maana naona umekuwa Naibu Waziri wa Michezo sasa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema kuhusiana taratibu na sheria ni pamoja na kupata ripoti kwa nini mchezo wa tarehe 8 Machi haukuchezwa?

**SPIKA:** Sasa wewe ndiyo ulikuwa unakataza ushabiki, sasa hapo ndiyo unataka ushabiki, haya wa Simba anayetaka kumjibu. Mheshimiwa Esther Matiko, mjibu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, lazima tuheshimu kanuni ambazo zina-*guide* mchezo wa mpira wa miguu tuweze kukuza vipaji, tusiweke ushabiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, sasa aulize swali lake.

Na. 575

**Kukuza Kilimo cha Parachichi – Ngara**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukuza kilimo cha parachichi Ngara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, mikakati inayotekelezwa katika Wilaya ya Ngara ni pamoja na kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa miche bora ya parachichi ambapo Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania *(TOSCI)* ilitoa elimu ya uzalishaji wa miche, kutoa elimu ya kilimo bora na udhibiti wa

visumbufu wa zao la parachichi na kuendelea kufungua masoko mapya ya parachichi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2023/2024 na 2024/2025 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilinunua na kusambaza bure miche bora ya parachichi 26,000 kwa wakulima. Pia katika msimu wa mwaka 2025/2026 Wizara ya Kilimo itashirikiana na halmashauri na sekta binafsi kuzalisha na kusambaza miche bora ya parachichi 100,000. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (*TPHPA*) imepanga kununua na kusambaza kiuatilifu maalum cha parachichi aina ya *copper sulphate* kwa lengo la kudhibiti magonjwa ya ukungu. Vilevile majaribio ya mbolea maalum za zao la parachichi yanaendelea ili viwanda vya ndani viweze kuzalisha mbolea hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Kwa kuwa kule Ngara tumeandaa vitalu vinne ambavyo vimepelekwa karibu na mahali ambapo wananchi wanaishi kwa ajili ya kuotesha miche ya kahawa; na kwa kuwa tayari kuna miundombinu ya kutosha inayo-*support* kuotesha miche ya kahawa huko vijijini. Hauoni kuna umuhimu wa hii miche sasa ya parachichi ikaoteshwa sambamba na ilipo miche ya kahawa ili iweze kuwafikia wananchi kwa uharaka na kwa urahisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Ndaisaba kwa kazi nzuri anayoifanya katika jimbo lake na nimthibitishie tu maoni yake tumeyapokea na tutayafanyia kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, kwa kuwa kilimo cha michikichi Kyela, Mkoani Mbeya hakifanyi vizuri ni upi mkakati wa Serikali kukifufua kilimo hiki na kukikuza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, moja ya mkakati wa Serikali kwa zao la mchikichi ambao tuko nao sasa hivi ni pamoja na kugawa mbegu bure kwa maeneo yote wanakolima michikichi ikiwemo Kyela na Kigoma na moja ya mlezi mkubwa wa zao hilo ni Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, tuna mipango kabambe kuhakikisha kwamba chikichi inakua nchini ili tuweze kuzalisha mafuta mengi hapa nchini na kupunguza uagizaji kutoka nje.

Kwa hiyo, jambo hili lipo katika mipango yetu na tuseme ni mipango endelevu ambayo tunaifanyia kazi sasa hivi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, upo mkakati wa kujenga mabwawa kwa ajili ya zao la kitunguu saumu Mbulu Vijijini; je, lini Serikali mtatangaza yale mabwawa ili mkakati ule ukamilike?

**SPIKA:** Hebu rudia swali.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mkakati wa kuendeleza zao la vitunguu saumu Mbulu Vijijini; Serikali itatangaza lini mabwawa ambayo yamewekwa kwenye mpango wetu ili zao hilo liweze kukolea Mbulu Vijijini?

**SPIKA:** *Wallah,* Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, niseme tu na Mheshimiwa Flatei hapa alikuwa anazungumzia tu miradi ya mabwawa ambayo ipo katika eneo lake na nimwambie tu ipo katika hatua mbalimbali. Ipo ambayo tunafanya upembuzi na usanifu wa kina, ipo ambayo

tumeshamaliza hiyo hatua na tupo katika hatua ya kutafuta mkandarasi. Kwa hiyo, tukishamaliza hizi hatua zote sasa hivi tutakabidhi wakandarasi *site* ili wakulima wa vitunguu saumu sasa waanze kulima kwa uhakika katika kipindi chote cha mwaka, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, wananchi wa Jimbo la Hai wamehamasika sana kulima zao la parachichi. Changamoto wanayokumbana nayo ni soko kwa wakati kiasi kwamba parachichi ambalo lilipaswa kuuzwa kilo shilingi 1,000, daraja la kwanza, kwa sababu ya kuchelewa linauzwa shilingi elfu tatu kwa kilo, kwa maana ya daraja la tatu, ambalo zamani walikuwa wanaita *reject*.

**SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuna soko la kutosha kwa wakati la zao la parachichi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimpongeze Mheshimiwa Saashisha kwa swali lake la msingi. Nimthibitishie tu miongoni mwa mikakati tuliyonayo sasa hivi ni kujenga tunasema *storage facilities* zile *cold chain storage facilities* kwa ajili ya uhifadhi wa parachichi hususani mkulima anapotoa shambani kabla ya kupata soko la uhakika. Kwa hiyo, huo ndiyo mpango mkubwa tulionao na tutafanya katika maeneo yote ambapo zao la parachichi linazalishwa.

Mheshimiwa Spika, lengo la pili la Serikali ni kuwa na masoko ya uhakika. Tumeshasaini mikataba na baadhi ya nchi kupeleka parachichi zetu nje ya nchi, lakini kuna kampuni nyingi ambazo tayari tumeshaingia nazo mkataba kupitia *COPRA* na tumeyagawa katika maeneo mfano hata Hai kuna kampuni kama GRIVIA zipo kule kwa ajili ya kununua parachichi. Kwa hiyo,

tutasisitiza tu wale wote tulioingia nao mikataba wafanye kazi hiyo kwa wakati, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, msichangie wakati wa maswali, uliza swali. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi. Kwa kuwa mazao yanayolimwa kwa mtindo wa kilimo hai yana soko zuri duniani. Je, nini mkakati wa Serikali kushajiisha na kuwaelimisha wananchi kulima parachichi kwa mtindo wa kilimo hai nchini kote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimpongeze Mheshimiwa Asha Abdullah Juma kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Spika, ninatambua ni mdau wa kilimo hai na kilimo hai ni kilimo ambacho hatutumii mbolea za kisasa tunatumia mbolea ya asili. Kwa hiyo, yapo mazao ambayo nchi hii tunalima kwa mfumo wa kilimo hai na moja ya mkakati wa Serikali ni kuhakikisha mfumo huu unaendelea na ndiyo maana pale Wizarani tumeshafungua dawati kwa ajili ya kilimo hai kuweza kusisitiza na kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kuingia katika kilimo hicho, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ni upi mkakati wa Serikali wa kuwasaidia wananchi wa Mbulu na Babati kwenye mazingira mazuri sana ya kuzalisha parachichi kupata mbegu nzuri ya parachichi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi, Mbulu, Babati na maeneo yote yanayolima parachichi yapo katika mkakati wa pamoja wa kugawa miche bure ya parachichi. Tunataka kupeleka mbolea

maalum kwa maana ya *copper sulphate* kwa ajili ya visumbufu vya zao la parachichi na ipo mikakati mingine mingi. Kwa hiyo, nimthibitishie tu ipo sehemu ya mkakati wa Serikali, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, ni upo mkakati wa Serikali kuboresha kitalu cha miche ya parachichi kilichopo Kilolo ambacho kilianzishwa na *TARI* na hakina ubora kwa sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, waambie tu wananchi wa Kilolo kwamba tumeshatenga fedha kwa ajili ya kile kituo na *TARI* ndiwo wataosimamia kwa ajili ya uzalishaji miche kwa ajili ya wananchi wake na Nyanda za Juu Kusini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mvomero wamehamasika sana kulima mazao haya kimkakati; je, Serikali inatoa kauli gani kwa *AMCOS* ambazo zinachukua mazao haya ya kimkakati na wanachelewesha malipo ya wananchi, kwa mfano tunayo *AMCOS* ya Mhonda Juu wanadaiwa zaidi ya shilingi bilioni mbili na mpaka sasa hivi ni zaidi ya wiki mbili hawajalipa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge, moja ya maelekezo ambayo sisi Wizara tulitoa ni kwamba wakulima wote wanapaswa kulipwa ndani ya siku saba mpaka 14 mara baada ya mazao yao kuuzwa. Kwa hiyo, kwenye kesi kama hizo ninaomba nilichukue na niende nikalifuatilie ili tuhakikishe hao wakulima wanalipwa kwa wakati, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta tangazo la wageni.

Kwanza tutaanza na wageni wenu; tunao wageni 57 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria, hawa ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi *St. Joseph Millenium* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga ambao ni walimu kutoka Mikoa ya Arusha na Rukwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna mgeni wa Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo, huyu ni rafiki yake kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 51 wa Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo ambao ni wanafunzi 48 na walimu watatu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Salvation kutoka Misungwi, Mkoani Mwanza. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ambaye ni Chifu Ndenjela Mwaigaga kutoka Uyole, Mkoani Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe ambaye ni ndugu yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Venant Daud Protas ambao ni marafiki zake kutoka Uyui, Mkoani Tabora. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Oran Manase Njeza ambaye anatoka Kata ya Ulenje, Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Singida na Mwanza. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao ni Wajumbe wa Baraza Kuu la Vijana Wilaya ya Kishapu, Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Innocent Bilakwate ambao ni viongozi wa Chama cha Walimu kutoka Wilaya ya Kyerwa, Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Charles Muguta Kajege ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Jacqueline Andrew Kainja ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi ambao ni walimu kutoka Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wanne wa Mheshimiwa Tunza Issa Malapo ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vilevile wapo wageni sita wa Mheshimiwa Joseph George Kakunda ambao ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Sikonge, Mkoani Tabora. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ambao ni walimu wastaafu wa Shule ya Sekondari Mawenzi kutoka Moshi Mjini, Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Ally Juma Makoa ambao ni wapiga kura wake kutoka Kondoa, Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 64 wa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo ambao ni wanafunzi 60 na walimu wanne wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Dkt. Asha-Rose Migiro kutoka Wilaya ya Mwanga, Mkoani Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 64 wa Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ambao ni wanafunzi 55 na walimu tisa wa Shule ya Awali na

Msingi Braggin kutoka Jimbo la Kibamba, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 20 na viongozi sita kutoka Shule ya Awali na Msingi Consalt ya Wilaya ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 50 na walimu watano wa Chama cha Skauti wa Shule ya Msingi Oysterbay na Shule ya Immaculate kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 6 Juni, 2025 katika Kikao cha 41 cha Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge, Mheshimiwa Felista Njau aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Njau alilalamika kwamba Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda - Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, hakujibu swali lake la nyongeza lilitokana na swali la msingi namba 526 la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma. Mheshimiwa Njau alitaka kujua kama suala hilo linaruhusiwa.

Mheshimiwa Felista Njau alilalamika kama ifuatavyo; "Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninauliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri hakuni-*address* swali langu kabisa, maana yake hakunijibu mimi, alikuwa anaongea, anAmtaja Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo. Ninafurahi akim-*address,* lakini nilikuwa ninaomba anijibu mimi kwa sababu sikutendewa haki. Hakunijibu swali langu alimu-*address* Mbunge wa Jimbo, akazungumza mwanzo-mwisho wala hakunijibu, na mimi nimetumwa na wananchi kwa mujibu wa Katiba, nina haki ya kupewa nafasi hiyo. Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako kama nimetendewa haki." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Felista Njau aliomba Mwongozo kupitia Kanuni ya 76 ambapo alitaka kujua kama suala hilo linaruhusiwa. Mheshimiwa Mwenyekiti aliyekuwepo wakati huo, Mheshimiwa

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, aliahidi kutoa Mwongozo baada ya kupitia *Hansard* na kujiridhisha juu ya malalamiko ya Mheshimiwa Njau.

Waheshimiwa Wabunge, *Hansard* zinaonesha kuwa swali la Mheshimiwa Njau lilikuwa kama ifuatavyo; "Kumekuwa na migogoro ya ardhi kati ya wawekezaji na wananchi katika Mkoa wa Kilimanjaro hasa Jimbo la Moshi Vijijini na imeonekana kuleta athari hasi kwa muda mrefu kwa sababu migogoro hii imedumu kwa muda mrefu bila suluhisho. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wanakwenda kutatua migororo hii ili wananchi waweze kuishi kwa amani? Ahsante sana."

Waheshimiwa Wabunge, swali hilo lilijibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri kama ifuatavyo; "Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Mbunge wa Jimbo hili amekuwa karibu sana na sisi kwa ajili ya kufuatilia namna ambavyo tunaweza kwenda kuimaliza hii migogoro na tunakumbuka kuna baadhi ya migogoro ambayo tayari tulishakutana na Mheshimiwa Mbunge, tumemwekekeza namna ya kwenda kuimaliza suala hili na tunapata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo na mimi nikuhakikishie tu Mheshimiwa Njau ukishirikiana vizuri na Mheshimiwa Mbunge wa jimbo." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitia *Hansard* nimeona kwamba katika swali lake la nyongeza Mheshimiwa Njau aliuliza swali kuhusu tatizo la uwepo wa migogoro ya ardhi baina ya wananchi na wawekezaji katika Mkoa wa Kilimanjaro hususani katika Jimbo la Moshi Vijijini. Mheshimiwa Njau alieleza kuwa migogoro hiyo inaleta athari hasi kwa wananchi wa mkoa huo. Hivyo, alitaka kufahamu Serikali ina mkakati gani katika kutatua migogoro hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, katika kujibu swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kuwa Serikali imekuwa ikitatua migogoro ya wawekezaji na wananchi katika mkoa huo na kwamba katika kufanya hivyo imekuwa ikishirkiana na Mheshimiwa Mbunge wa jimbo ambaye amekuwa anatoa ushirikiano mkubwa. Aidha, Mheshimiwa Naibu Waziri alimwomba Mheshimiwa Njau

kushirikiana na Mbunge huyo wa Jimbo la Moshi Vijijini ili kwa pamoja wafikie suluhu ya kudumu ya migogoro hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, suala linalotakiwa kutolewa Mwongozo ni je, majibu ya Mheshimiwa Waziri yalijielekeza kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Njau na je, Mheshimiwa Njau alijibiwa swali lake la nyongeza kikamilifu?

Waheshimiwa Wabunge, kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge zinaonesha kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza baadhi ya hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kumaliza migogoro hiyo kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini. Aidha, katika ushirikiano alieleza kuwa kuna masuala ambayo Mbunge wa Jimbo alikubaliana na Serikali kuyafanyia kazi, kwa nia hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri alimuomba Mheshimiwa Njau kushirikiana na Mbunge wa jimbo katika kuhitimisha migogoro hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa kuomba Mwongozo Mheshimiwa Njau alilalamika kuwa yeye kama Mheshimiwa Mbunge hakutendewa haki na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kitendo chake cha kumtaja Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini tena kwa zaidi ya mara moja wakati akijibu swali lake. Aidha, alifafanua kwamba Wabunge wote iwe waliochaguliwa kuwakilisha majimbo ya uchaguzi, Wabunge wa Viti Maalum, Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wabunge wa Kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wote wanatambuliwa kuwa sawa kwa mujibu wa Ibara ya 66 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Hivyo, wote wana haki sawa katika kuuliza maswali, na kupata majibu yanayojitosheleza kwa maswali wanayouliza.

Waheshimiwa Wabunge, *Hansard* zinaonesha kuwa ni kweli Mheshimiwa Waziri katika majibu yake alimtaja Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo zaidi ya mara moja. Nilivyoona, Naibu Waziri alifanya hivyo siyo kwa nia mbaya, bali kufafanua namna Serikali inavyoshirikiana na Mbunge huyo wa Jimbo katika kushughulikia migogoro ya ardhi katika Jimbo la Moshi Vijijini baina ya wananchi na wawekezaji na katika kuthibitisha hilo Mheshimiwa Naibu Waziri

alimuomba Mheshimiwa Njau ashirikiane na Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini ili kupata suluhu ya migogoro hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri ukienda moja kwa moja kwenye swali alilokuwa ameuliza Mheshimiwa Felista Njau zaidi ya Mheshimiwa Naibu Waziri kueleza kwamba Serikali inashirikiana na Mbunge wa Jimbo na pili kwamba Mbunge muuliza swali ashirikiane na Mbunge wa Jimbo, hayo ndiyo yalikuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Hivyo basi, swali lililoulizwa na Mheshimiwa Felista Njau halikujibiwa na Naibu Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mbunge wa Viti Maalum ana haki sawa na Mbunge mwingine kuuliza swali, lakini mapendekezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri kushirikiana kati ya Wabunge yako sawa sawa ila Mbunge wa Viti Maalum alipaswa ajibiwe swali alivyouliza yeye kwa niaba ya wananchi wake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo Mwongozo wa Kiti, sasa kwa sababu lilikuwa ni swali la nyongeza na Kanuni zetu zinasema kama swali la nyongeza halikujibiwa kikamilifu linapaswa liletwe kama swali la msingi.

Kwa hiyo, kiti hakiwezi kuagiza kwamba swali lijibiwe upya isipokuwa kinamwagiza Mheshimiwa Mbunge kama bado anataka majibu ya swali lake la nyongeza alilete kama swali la msingi ili Mheshimiwa Waziri aweze kupata nafasi ya kujibu swali hilo kikamilifu. Huo ndiyo Mwongozo wa Spika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA KAMATI

### Azimio la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Bunge

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aje awasilishe Taarifa ya Kamati ya Kanuni za Bunge kama ambavyo iliwekwa mezani, Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KANUNI ZA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Kanuni za Bunge kuhusu Mapendekezo na Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023.

Mheshimiwa Spika, utangulizi; nitumie nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali kwa ujumla kwa ushirikiano wanaolipatia Bunge letu na sisi viongozi wa Bunge na Wabunge wote kwa ujumla katika kutekeleza majukumu yetu ya Kibunge. Hakika ushirikiano huu unaliwezesha Bunge hili kutekeleza majukumu yake kwa wepesi na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako thabiti katika kuliendesha Bunge letu katika kipindi chote cha uongozi wako. Vilevile ninakushukuru kwa utayari wako ulioiwezesha Kamati kuchambua kanuni na kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya kanuni ili ziweze kusaidia uendeshaji bora wa kanuni katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 176(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kanuni za Bunge kuhusu Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imeundwa chini ya Kanuni ya 137 na majukumu yake yamefafanuliwa katika fasili ya (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Mojawapo ya jukumu la Kamati ni kujadili na kupendekeza maboresho ya Kanuni za Kudumu za Bunge kama ilivyoainishwa katika fasili 3(3)(a).

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi huo Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto ya matumizi ya kanuni, kasoro za kiuandishi na uhitaji wa kuweka masharti mapya ambayo ni muhimu katika uendeshaji wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu naomba sasa kuwasilisha mapendekezo ya maboresho ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambayo iwapo Bunge litaridhia na kupitisha kwa njia ya azimio zitatumika katika Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mapya ambayo hayakuwepo kwenye kanuni hivyo Kamati inapendekeza yawekwe kwenye kanuni. Vilevile yapo maeneo yaliyokuwepo kwenye kanuni ambapo inapendekezwa yafanyiwe maboresho. Mapendekezo yanayoletwa kwenu ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, maeneo mapya yanayopendekezwa ahadi ya uzalendo; baadhi ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola katika vikao vyake yanao utaratibu wa Wabunge kutoa ahadi ya uzalendo. Hivyo, inapendekezwa tuweke utaratibu huu katika kanuni ambapo Wabunge watatoa ahadi ya uadilifu katika kila Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Bunge ambapo kila Mbunge ataahidi kuwa mtiifu na mwaminifu kwa nchi yetu na kufanya kazi kwa uadilifu.

Mheshimiwa Spika, kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais; Bunge huthibitisha Makamu wa Rais baada ya uteuzi wake. Kanuni zetu hazijaweka utaratibu wa kumthibitisha Makamu wa Rais anayeteuliwa katika kipindi tofauti na Uchaguzi Mkuu. Inapendekezwa kuweka utaratibu huu katika kanuni.

Mheshimiwa Spika, Taarifa za Kamati za Hesabu na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma; Bunge linao utaratibu wa Kamati

ya Hesabu za Serikali Kuu, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma huwasilisha taarifa katika Mkutano wa mwezi Oktoba-Novemba. Kwa kuwa utaratibu huu haukuwepo kwenye kanuni tunapendekeza kuwekwa utaratibu huo sasa.

Mheshimiwa Spika, kura ya kutokuwa na upande *(abstention);* wakati wa kupitisha bajeti, baadhi ya Wabunge wamekuwa wakipiga kura ya *abstention* kura hiyo haijawekewa masharti katika kanuni na hivyo haikuwa inahesabiwa. Tunapendekeza kuboresha kanuni kwa kuitambua kura hiyo ili ihesabiwe.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Spika na Wabunge wote; upo utaratibu wa Bunge kuwa na Mkutano wa Spika na Wabunge wote kujadili masuala ya kibunge kabla ya Mkutano wa Bunge na Waziri Mkuu. Kwa kuwa mkutano huo haupo kikanuni inapendekezwa utaratibu huo utambuliwe rasmi na kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, kusoma Bajeti Kuu ya Serikali; Bajeti Kuu ya Serikali imekuwa ikisomwa saa 10.00 jioni lakini utaratibu huo haupo kwenye kanuni. Inapendekezwa yafanyike marekebisho ili kanuni ieleze kuwa bajeti hiyo itasomwa saa 10.00 jioni. Utaratibu huu utaendana na makubaliano ya nchi wanachama Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kusoma bajeti kwa pamoja katika wakati huo.

Mheshimiwa Spika, maeneo yanayofanyiwa maboresho; utambulisho wa wageni Bungeni; utambulishaji wa wageni huchukuwa muda mrefu wa Bunge hivyo kuathiri muda uliotolewa kwa shughuli za Bunge. Inapendekezwa marekebisho ya kanuni yafanywe ili utambulisho ufanyike kwa wageni wa kitaifa, kimataifa pamoja na wageni waliotoa mchango wa Taifa pekee.

Mheshimiwa Spika, upeperushaji wa bendera za Bunge; inapendekezwa kuboresha masharti ya upeperushaji wa bendera katika magari ya Wabunge kwa nia ya kuwapa heshima ambayo Wabunge wanastahili. Hivyo, inashauriwa kuboresha masharti

hayo ikiwa ni pamoja na Wabunge kutokupeperusha bendera zaidi ya moja kwenye gari la Mbunge kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, mavazi rasmi ya Bunge; inapendekezwa kuwekwa masharti yanayozuia Wabunge, watumishi wa Bunge na wageni wakiwa Bungeni kuvaa mavazi yenye mwelekeo wa ushabiki au wapenzi wa chama fulani yenye alama, nembo, maandishi, jina au misemo ya vyama. Mapendekezo haya yanakusudia kudumisha dhana ya Bunge kuwa huru na lenye umoja bila kujali itikadi za kisiasa.

Mheshimiwa Spika, fomu za uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki; wagombea wa nafasi ya Ubunge wa Afrika Mashariki hutakiwa kujaza fomu za maelezo binafsi ya mgombea. Fomu hizo hazipo kwenye kanuni, hivyo inapendekezwa kuziweka fomu hizo katika kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine ya maboresho yanahusu kuunganisha maudhui yanayofanana, lakini yamewekwa katika kanuni tofauti, kuongeza tafsiri ya misamiati ambayo haijatafsiriwa na kuandikwa baadhi ya maeneo katika lugha fasaha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa hii Kamati imeandaa rasimu yenye mapendekezo na maboresho kwa kila kanuni na kila fasili ya nyongeza za kanuni ambayo imewekwa kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho kwa mara nyingine nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kanuni za Bunge kwa kujituma katika zoezi la kuandaa mapendekezo ya marekebisho haya naomba majina yao yaingie katika *Hansard* ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kuishukuru Sekretarieti ya Kamati chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa utaalamu na uratibu wa shughuli za Kamati hadi kufanikisha na kukamilisha kazi hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha nitumie fursa hii kuishukuru familia yangu na wapiga kura wangu wa Jimbo la Ilala kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa katika kipindi chote tangu waliponichagua, hakika najivunia mafanikio ambayo kwa pamoja tumeyatapa. Tuendelee kushirikiana katika kuleta maendeleo zaidi katika Jimbo la Ilala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati ijadiliwe mapendekezo ya marekebisho na baadaye kupitishwa kwa njia ya azimio; kanuni zinazopendekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KANUNI ZA BUNGE KUHUSU MAPENDEKEZO YA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA KUDUMU ZA BUNGE, TOLEO LA FEBRUARI, 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote, nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Serikali kwa ujumla kwa ushirikiano waliotupatia sisi viongozi wa Bunge na Wabunge wenzetu katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi kipindi chote cha uhai wa Bunge la Kumi na Mbili.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza kwa utayari wako uliowezesha Kamati ya Bunge kupitia kanuni na kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya baadhi ya Kanuni. Mapendekezo hayo yanalenga kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kipindi ambacho kanuni hizo zimekuwa zikitumika.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, nikupongeze kwa dhati kabisa kwa maono na ubunifu wako katika kubuni mbinu mbalimbali za uendeshaji wa shughuli za Bunge na

hasa katika mazingira ambayo kanuni zetu hazikutoa Mwongozo. Ni ukweli usiofichika kwamba ubunifu wako umetuwezesha kukabiliana na changamoto mbalimbali za uendeshaji wa Bunge,

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 176 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kanuni za Bunge kuhusu Marekebisho au mabadiliko katika Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Msingi wa taarifa hii ni Kanuni ya 137 iliyoanzisha Kamati na kufafanua majukumu yake kwenye fasili ya 3 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge ambapo miongoni mwa majukumu ya Kamati ya Kanuni za Bunge ni kujadili na kupendekeza maboresho ya Kanuni za kudumu za Bunge kama ilivyotajwa katika fasili ya 3(3)(a) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi naomba kuwasilisha mapendekezo ya maboresho ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho zilipitishwa na Bunge mwezi Juni, 2020. Kanuni hizo zilirekebishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni mwaka 2023, hivyo Toleo la Februari, 2023 lilichapishwa. Kanuni hizo zilianza kutumiwa rasmi na Bunge hili la Kumi na Mbili. Kwa kuwa Bunge hili linaelekea mwisho wa kipindi cha uhai wake, imeonekana ni muhimu kuzipitia Kanuni hizi kwa lengo la kuziboresha ili zitumike wakati wa Bunge la Kumi na Tatu litakaloanza Novemba, 2025. Utaratibu huu ni wa kibunge na huzingatiwa na mabunge mengine ya Jumuiya za Madola.

## 2.0. JINSI KAMATI ILIVYOFANYA KAZI

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu la Kamati ya kuandaa mapendekezo ya maboresho ya Kanuni. Njia zifuatazo zilitumika.

(a) Kupitia Toleo la Februari, 2023: kupitia kanuni moja baada ya nyingine pamoja na Nyongeza za kanuni ili kuainisha maeneo yanayohitaji maboresho;

(b) Kubaini mambo mapya ambayo Kamati iliona upo umuhimu wa kuyajumuisha katika marekebisho ya Kanuni hizi.

(c) Kujifunza uzoefu kutoka katika Bunge ya nchi nyingine.

(d) Kupokea maoni kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na kuyafanyia kazi.

(e) Kufanya utafiti kuhusu matumizi ya kanuni.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilisha kazi ya uchambuzi, Kamati iliainisha changamoto, mapendekezo na manufaa ya pendekezo kwa kila kanuni.

## 3.0. MAENEO YALIYOFANYIWA MAREKEBISHO KATIKA KANUNI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini uwepo wa maeneo mbalimbali katika Kanuni yenye changamoto zinazohitaji kupatiwa ufumbuzi wa kanuni. Maeneo yenye changamoto ni kama ifuatavyo: -

### 3.1. Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge na Wajumbe wa Tume

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa katika Kanuni zilizopo haujabainishwa utaratibu katika Kanuni unaosimamia uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge na Wajumbe wa Tume katika mazigira ambayo idadi ya majina ya wagombea inalingana na nafasi zilizopo.

Utaratibu wa kupiga kura unaotakwa katika Kanuni ya 92 umekuwa unatumika unaozingatia Uamuzi wa Bunge unaotokana na Spika hulihoji Bunge ambapo Wabunge huitikia kwa pamoja kwa sauti za wanaafiki au wasioafiki.

Hivyo, Kamati inapendekeza kufanya marekebisho ya kanuni ili kuweka masharti yatakayowezesha uchaguzi wa Wenyeviti katika mazingira hayo.

3.2. **Nafasi Wazi ya uwakilishi wa Wabunge katika vyombo vingine**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliona kuwa Kanuni ya 16 kuhusu nafasi wazi ya uwakilishi wa Wabunge haizungumzi mazingira ya mjumbe kujiuzuru au kufariki kama sababu za kuacha wazi nafasi ya uwakilishi. Hivyo, inapendekezwa kuboresha kanuni ya 16 ili kuongeza sababu hioz ili kuwa sababu zinazosababisha nafasi kuwa wazi.

3.3. **Ahadi ya Uzalendo**

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola yanao utaratibu wa Wabunge kutoa ahadi ya uzalendo katika vikao vyake. Hivyo, inapendekezwa tuweke utaratibu huo katika Kanuni ambapo Wabunge watatoa ahadi ya uadilifu katika kila Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Bunge ambapo kila Mbunge ataahidi kuwa mtiifu na mwaminifu kwa nchi yetu na kufanya kazi zake kwa uadilifu.

Aidha, uzoefu wa nchi nyingine za Jumuiya ya Madola, unaonesha kuwa Wabunge hutoa Ahadi kwa nchi na Wananchi wake. Ahadi hii hutolewa kabla ya kuanza vikao vya Bunge. Ahadi hiyo humaanisha kuwa, Wabunge watakuwa wazalendo wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kibunge. Kwa kuwa utaratibu huu haupo katika Bunge letu, Kamati inaona kuwa ni muhimu kuiga utaratibu huu mzuri.

3.4. **Kupiga kura wakati wa kupitisha Bajeti ya Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** kanuni hazijatambua utaratibu wa kuweka kumbukumbu ya kura za Wabunge wanaotumia neno *abstain* kupiga kura zao. Kutokana na kutotambulika katika kanuni kwa kura hiyo, imekuwa ni changamoto katika uwekaji wa taarifa za zoezi la kupiga kura. Hivyo, inapendekezwa suala hili lisimamiwe katika Kanuni ili kurekodi kura hiyo ya *abstain.* Vilevile inapendekezwa kuitambua kura hiyo

kwa maneno **Sipigi Kura** ambayo ni tafsiri ya neno hilo katika lugha ya Kiswahili.

3.5. **Muda wa Kusoma Bajeti Kuu ya Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** uzoefu umeonyesha kuwa Bajeti Kuu ya Serikali imekuwa ikisomwa saa 10:00 Jioni lakini muda wa kusoma Bajeti haupo katika kanuni ya 124 inayosimamia suala hilo. Kamati inapendekeza yafanyike marekebisho ili kutambua muda wa kusoma Bajeti ya Serikali kwamba itakuwa ni Saa 10:00 jioni lakini vilevilie kuwezesha kuendana na makubaliano ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kusoma Bajeti zao Kuu za Serikali kwa pamoja wakati huo.

3.6. **Mkutano wa Spika na Wabunge Wote**

**Mheshimiwa Spika,** upo utaratibu wa kuwa na Mkutano wa Spika na Wabunge wote unaojadili masuala ya kibunge kabla ya Mkutano wa Wabunge na Waziri Mkuu ambao umetajwa katika kanuni ya 130 ya Kanuni. Mkutano unaoitishwa na Spika kujadiliana na Wabunge kuhusu masuala ya kibunge haujatajwa katika kanuni, hivyo inapendekezwa Mkutano huo utambuliwe rasmi na Kanuni.

3.7. **Taarifa za Kamati za Hesabu na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 136(15) Kamati za Bunge hutakiwa kuwasilisha Taarifa za Kamati wakati wa Mkutano wa Bunge wa Mwezi Januari-Februari. Bunge linao utaratibu wa Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma huwasilisha Taarifa za Mwaka katika Mkutano wa Mwezi Oktoba-Novemba. Utaratibu huo haujawekwa katika Kanuni. Kutokana na umuhimu katika kusimamia fedha na mitaji ya umma, Kamati inapendekeza utaratibu huo wa kuwasilisha Taarifa uwekwe katika Kanuni.

3.8. **Utambulisho wa Wageni Bungeni**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Bunge zimeweka utaratibu wa kutambulisha wageni Bungeni. Hata hivyo, utambulishaji wa wageni umeonekana kuchukuwa muda mwingi wa Bunge jambo hilo linalopunguza muda uliotengwa kwa Shughuli za Bunge. Kamati inapendekeza kufanya marekebisho ya kanuni ya 161 kwa lengo la kuokoa muda wa Shughuli za Bunge kwa kutambulisha wageni mahusis wa kitaifa na kimataifa waliopo katika Ukumbi wa Bunge pamoja na wageni waliotoa mchango wa kitaifa unaohitaji kuenziwa.

3.9. **Upeperushaji wa Bendera ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika,** Wabunge wanaruhisiwa kupeperusha Bendera ya Bunge katika ofisi zao na katika magari yao binafsi. Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya matumizi yasiyo sahihi ya Bendera yanayosababisha kushusha hadhi na heshima ya Mbunge. Hivyo, inapendekezwa kuweka masharti ya kusimamia upeperushaji wa Bendera katika gari la Mbunge. Mapendekezo hayo ni ya kumzuia Mbunge kupeperusha Bendera akiwa anaendesha gari lake, Mbunge kutopeperusha katika gari lake Bendera zaidi ya moja kwa wakati mmoja na vilevile kuelekeza kuwa Mbunge anapaswa kupeperusha bendera akiwa ameketi upande wa kushoto wa gari lake likiwa linaendeshwa na dereva.

3.10. **Utaratibu Wakati wa Kuridhia Mkataba wa Kimataifa**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 110 imeweka utaratibu wa Bunge kujadili na kupitisha Azimio Kuridhia ua Kutoridhia Mkataba wa Kimataifa. Utaratibu huo umeeleza jinsi Hoja itakavyowasilishwa na Msemaji wa Serikali bila kueleza nafasi ya kutoa maoni ya Kamati ya Bunge iliyofanya uchambuzi na vilevile Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni. Kamati imependekeza kuongezwa kwa kanuni ndogo mpya katika kanuni ya 110 inayoweka sharti kwa Mwenyekiti wa Kamati

iliyoshughulikia Mkataba pamoja na Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni kutoa maoni yao kabla ya Wabunge kujadili na kufanya uamuzi kuhusu Mkataba husika.

3.11. **Kuthibitisha Uteuzi wa Makamu wa Rais**

**Mheshimiwa Spika,** Inapendekezwa kuwa na kanuni mahsusi inayoeleza utaratibu wa Bunge wa kuthibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais pale inapotokea ameteuliwa baada ya kipindi cha uchaguzi kupita (Ibara ya 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977). Utaratibu unaopendekezwa unatokana na uzoefu wa Bunge letu kuendesha mchakato kama huo.

3.12. **Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kamati Teule**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 139(4) imeelekeza kuwa Spika atachagua Wajumbe wa Kamati Teule. Kanuni ya 140 imeelekeza namna Mwenyekiti takavyoitisha vikao na kuongoza vikao. Kanuni hizo hazijaweka utaratibu wa lini, wapi na namna ambayo Mwenyekiti wa Kamati hiyo atakavyochaguliwa. Katika eneo hili, Kamati inapendekeza kuboresha kanuni ndogo ya (4) ya kanuni ya 139 ili kuweka sharti kwa Wajumbe wa Kamati kukutana mara baada ya kuteuliwa ili kumchagua Mwenyekiti kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao.

3.13. **Majukumu ya Katibu wa Kamati Maalum**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni zimeweka utaratibu wa uundaji wa Kamati mbalimbali zikiwemo Kamati Teule na Kamati Maalumu. Kamati inapendekeza kuongeza kanuni ndogo mbili mpya kwenye kanuni ya 144 zitakazobainisha majukumu ya Katibu wa Kamati hiyo kuhusu kutunza kumbukumbu za mahudhurio zitakazosainiwa na Mwenyekiti na kuambatishwa pamoja na Taarifa ya Kamati. Kwa mabadiliko hayo, majukumu ya Katibu wa Kamati Teule katika kanuni ndogo za (5) na (6) za kanuni ya 141 yatashabihianana

Kamati Maalumu kuhusu kutunza kumbukumbu na kutia saini kumbukumbu hizo.

3.14. **Mavazi Rasmi kwa Katibu na Wasaidizi Wanawake**

**Mheshimiwa Spika,** Mavazi rasmi kwa Katibu na Wasaidizi wake yameelezwa katika kanuni ya 170(5). Imeonekana kuwa, kwa upande wa wasaidizi wanawake, wapo wanaohitaji kuvaa vazi la ziada kwa misingi ya Imani zao lakini vazi hilo halijaorodheshwa katika mavazi rasmi. Kamati inapendekeza kuongeza kilemba cha kadri au mtandio kuwa sehemu ya vazi rasmi kwa Katibu au Msaidizi Mwanamke ambaye masharti ya Imani yanamtaka kuvaa vazi hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile katika kusimamia mavazi rasmi ya wabunge, imebainika kuwa baadhi ya wanaoingia maeneo ya Bunge huvaa sare zinazoshiria au kuzoeleka kuvaliwa na wafuasi au mashabiki wa vyama vya siasa kwa alama, nembo, maandishi ambavyo hutafsiriwa kwa jina, alama, msemo au nembo ya chama. Inapendekeza kuweka Kanuni inayokataza mavazi hayo ili kudumisha dhana ya Bunge kuendesha shughuli zake kwa uhuru na umoja bila kujali itikadi za kisiasa. Aidha, Kanuni kuhusu mavazi imeboreshwa ili kuweka usimamizi madhubuti wa mavazi Bungeni.

3.15. **Fomu za Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki**

Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki huwataka wagombea kujaza Fomu maalumu ili kutoa maelezo yao binafsi**.** Masharti hayo yameainishwa katika fasili ya 5(2) ya Nyongeza ya Tatu ta Kanuni lakin fomu hizo hazipo kwenye Kanuni. Hivyo, inapendekezwa kuziweka Fomu Maalum kwa ajili hiyo katika Kanuni.

3.16. **Marekebisho kwa kuandika lugha fasaha ya Kiswahili**

Kamati inapendekeza kufanyika maboresho machache ya kiuandishi baada ya kubaini uwepo wa

baadhi ya maeneo yanayohitaji kufanyiwa maboresho ya kiuandishi. Maboresho hayo yamezingatia misingi ya uandishi wa sheria. Vilevile, zoezi hili lilifanyika kwa kuhamisha, kuunganisha maudhui yaliyokuwa kaytika kanuni tofauti ili kuweka mpangilio mzuri wa maudhui ya Kanuni. Hivyo, inapendekezwa maboresho kufanyika ili kuwezesha kanuni kusomeka katika lugha sanifu.

## 4.0. SEHEMU YA TANO: HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho au maboresho ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Napenda nitumie nafasi hii tena kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi katika kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi tunaowawakilisha sisi Wabunge ndiyo kipaumbele cha kwanza na cha muhimu

Mhe. Spika kipekee nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini Kanuni zetu na kubaini maeneo tunayoyapendekeza ili Kanuni hizo ziweze kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Shughuli za Bunge. Kwa heshima naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati hii kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb.
2. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb.
3. Mhe. William Vangimembe Lukuvi, Mb.
4. Mhe. Hamza Saidi Johari, Mb.
5. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb.
6. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb.
7. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb.
8. Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb.
9. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
10. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb.
11. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb.
12. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb.

13. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb.
14. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb.
15. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb.
16. Mhe. Ally Mohamed Kassinge, Mb.
17. Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mb.
18. Mhe. Anton Albert Mwantona, Mb.
19. Mhe. Martha Nehemia Gwau, Mb
20. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb.
21. Mhe. Asha Abdullah Juma, Mb.
22. Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb.
23. Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest Mb.

Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge Ndugu Baraka I. Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, nawashukuru Ndg. Pius T. Mboya Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria, Ndg. Joshua Chamwela Mkurugenzi wa Idara ya Shughuli za Bunge, Ndg. Ruth S. Makungu Mratibu wa Ofisi ya Katibu wa Bunge, Ndg. Leocardo E. Kapongwa na Ndg. Agnes I. Ndumbati, *ndc* Wakurugenzi Wasaidizi Idara ya Huduma za Sheria. Vilevile ninawashukuru Ndg. Ludovick Ringia, Ndg. Maria Mdulugu, Ndg. Elizabeth Malogo na Ndg. Victor Kweka Makatibu wa Kamati na Ndg. Jenipha E. Ndagwa Mwandishi Mwendesha Ofisi na Ndg. Mainda Kifua Msaidizi wa Ofisi kwa kuratibu vema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali, lijadili mapendekezo haya ya marekebisho au maboresho ya Kanuni na baada ya hapo liazimie kupitisha Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb)
**MAKAMU MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA KANUNI**

11 Juni, 2025

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono ahsanteni sana.

Sasa sijapokea bado majina ya watu ambao wanataka kuchangia hoja hii na wengine sijajua kama walikuwa wanatafakari ama hakuna michango.

Kwa hiyo, niendelee na hatua zinazofuata? Aah Mheshimiwa, haya wale wanaotaka kuchangia wasimame ili nikishawaona, msimame hivyo hivyo mpaka nikutaje jina, haya.

Haya ahsanteni sana, tutaanza na Mheshimiwa Francis Mtinga atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Kasalali Mageni ajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika jambo muhimu kabisa la kanuni na taratibu ambazo zinalenga kuboresha shughuli za Bunge letu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mambo yote yaliyosemwa ni mema, ni mazuri, lakini nilikuwa naomba jambo moja tuliangalie vizuri kwa makini zaidi suala la kutokutambulisha wageni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ni nafasi nzuri sana ambayo Bunge hili limeiweka na sisi tumeikuta ambayo inatufanya kushirikiana na wananchi wetu kuliona Bunge lao, kulisikia Bunge lao, kuwawakilisha wale wananchi wengi ambao wachache wanapokuja hapa hujisikia kwamba kweli sisi ndio tunaowawakilisha.

Mheshimiwa Spika, wanapokuja hapa halafu wasitambulishwe na wenzao kule kwenye majimbo yetu wakawaona kwamba kweli wamefika Bungeni na kuwapelekea salamu jambo hilo kwa kweli linakuwa lina uzito sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikuombe wewe pamoja na kamati yako jambo hili najua mlitumia muda mrefu kulitafakari, lakini niwaombe mrudi nyuma kwamba hili suala la kutambulisha wageni libaki kama lilivyokuwa kwa sababu ni suala zuri sana katika kutufanya sisi na wananchi wetu tuweze kushirikiana katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mheshimiwa Anatropia Theonest ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwanza niseme nimeunga mkono na niipongeze Kamati kwa yale ambayo wameyazungumza, lakini nina mambo machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni hili suala la wageni. Mimi ninashauri wageni kwa kweli imekuwa ni wengi sana kiasi kwamba wanatulia muda kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, mimi nilikuwa ninashauri utaratibu ambao umependekezwa ni utaratibu ambao unafaa kabisa wa watu kusomwa tu kwamba kuna wageni fulani basi, lakini kwa kweli tukifanya hii kazi; kwa nini nazungumza hivi? Kwa sababu kuna watu tumejifunza muda mwingine wanatamani kuja kuoneshwa kwamba mimi natoka kampuni fulani, kwa sababu nafanya nini; yaani inaoneshwa kama ni sehemu ya *promotion* na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa heshima ya Bunge, tulikuwa tunatamani mtu kama ni wageni wanakuja hata kipindi ambacho siyo cha *session* la Bunge linaendelea wageni wanaweza wakaja hapa na wakafanya shughuli zao zingine za kuangalia, siyo lazima wakati wa *session* tu, lakini wakati wa *session* mimi nilikuwa nashauri kama watu wanakuja tuangalie jinsi gani ya kulinda muda, huu muda utumike kwa ajili ya shughuli zingine ambazo ni *special* kwa ajili ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kingine ni kwenye mavazi rasmi ni kitu muhimu sana kuhakikisha kwamba ndani ya Bunge sisi Bunge

hususan hata kwenye wakati wa Kamati za Bunge, ukiangalia wageni wanaotoka nje kuja kukutana na Wabunge pia kuna mtazamo ambao pia wanatazama heshima na uvaaji wa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatamani uvaaji wa mavazi rasmi ni kitu muhimu sana kwenye shughuli za Bunge ili kulinda heshima, taswira na muonekano wa Bunge kwa sababu muda mwingine Wabunge wanapokuja uvaaji wao kwenye matukio makubwa kama ya Kamati ambapo Kamati pia ni Kikao cha Bunge. Unakuta kabisa kwa kweli kinashusha heshima na hadhi ya Bunge letu. Kwa hiyo, ni muhimu sana kama Bunge tuliangalie hilo uvaaji lazima uendane na muonekano na heshima ya hadhi ya Bunge la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndio maoni yangu ambayo nilikuwa natamani nishauri kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaunga mkono hiki ambacho wenzetu wamesema. Ningetamani sana siku zingine nilifikiria kwamba humu ndani kuna *seating arrangement* ya Wabunge wa Upinzani wanapokaa, Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi na Serikali. Kuna ule upande wa Serikali kule nilitamani kwamba ubaki kuwa ni upande wa Serikali, Wabunge wakae upande mmoja ili wakati mwingine ambapo Wabunge wanachangia waangalie kama Serikali yao ipo au haipo humu ndani, ili wakati mwingine wanakuwa wamechangamana hapa Wabunge na Serikali unakuwa unashindwa kugundua ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *seating arrangement* ya humu ndani Wabunge tungekuwa na upande wetu rasmi na hawa wenzetu wa Serikali wabaki hapa ili nao wajue umuhimu wa wao kukaa Bungeni wakati shughuli za Bunge zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo yalikuwa ni maoni yangu na nikushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na nafasi hii ya kuchangia kanuni zinazokuja kuendesha Bunge lijalo.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza ambacho nilitamani sana tukiweke sana ni hili suala la wageni wanaokuja Bungeni kutokutambulishwa. Mimi nadhani ilivyo sasa ipo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wageni wanaokuja Bungeni na nadhani mpaka tutake kubadilisha ina maana kuna tatizo kubwa sana, lakini mimi sijaliona. Nadhani kwamba ni tatizo kubwa sana kutambua watu waliokuja kututembelea wageni wa Wabunge, wageni wa watu mbalimbali na nadhani hili sio kwamba ni matangazo. Bunge hili ni la Watanzania na sisi ni wawakilishi wao, tunawakilisha makundi mbalimbali ya wafanyabiashara, wakulima, wafugaji, madhehebu ya dini kila aina. Kwa hiyo, humu ni uwakilishi wa Watanzania. Mtu akija humu atatambulishwa nadhani haiwezi kuleta shida kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi bado ninapendekeza ibaki kama ilivyo sasa kwa sababu haijatuletea shida yoyote na nadhani ina tija zaidi kwa watu kujisikia kwamba pia na wao ni sehemu ya jumba hili la kidemokrasia nchini. Wakija hapa wajisikie wamekuja na wametambuliwa na kila mmoja apate hamu ya kuja, ndio maana vimewekwa vile viti watu waje, wapate hamu ya kuja kusikiliza na kujifunza kuhusu Bunge na waendelee kuwa wazalendo na kulipenda Bunge lao. Kwenye hili nilitaka kuchangia hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine sijui itakuje lakini kuhusu mavazi kuna kitu kinaitwa mavazi rasmi, lakini mavazi yetu rasmi mara nyingi yamekuwa ni mavazi ya kimagharibi, hasa kwa wanaume. Mimi binafsi ungeniuliza hivi nilivyojiniga na tai napata tabu sana, lakini ni humu tunaambiwa mavazi rasmi ni hayo.

Mimi nafikiri mavazi nadhifu tunayo mashati yetu ya Kiafrika mazuri, tunaweza kuvaa. Kuna makabila yanaheshimika kama Wamasai wana mavazi yao yale ya heshima tunaweza kuvaa, lakini sijui mavazi sijui; kama naona kama kuna ukoloni fulani hivi

na hizi tai na suti. Wale wenzetu Ulaya kwa sababu ya baridi na nini, ilifika wakati yakawa ndio mavazi yao nadhifu ili badala asijifunge na majipujipu, koti wakatengeneza inabana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi hapa navyokuwa hapa nalazimika kila siku nikija na tai nibanwe hivi inakuwa kidogo wakati mwingine tunapata shida. Mimi nafikiri suala la mavazi pia nalo liangaliwe hasa kwetu sisi wanaume, tusilazimike tu kuvaa mavazi ya aina fulani bado Watanzania wana mavazi yanayoheshimika, yatambuliwe na yaonekane yanaweza kuvaliwa ili twende pia hili Bunge ni la Kitanzania, Bunge la Kiafrika na Uafrika wetu ni muhimu sana na sisi pia tunatakiwa tuuze mavazi yetu ifike wakati hata huko Ulaya na wao watamani kuvaa nadhifu kama tunavyovaa sisi katika makabila yetu na tamaduni zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani hilo ni jambo la muhimu sana na nilifikiri kwenye hayo mawili kwa namna ambavyo tunaenda kurekebisha kanuni na kwa sababu ya uharaka na jambo lenyewe limekuja hivi tuone namna ya kuyaweka hivyo.

Mheshimiwa Spika, nakushuruu sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest atafuatiwa na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, moja nichangie katika kifungu cha 32(1) ambacho kimezalishwa kifungu kipya kinachoitwa Ahadi za Uzalendo.

Mheshimiwa Spika, nadhani hichi ni moja kati ya kifungu bora kabisa cha Mbunge ambacho Mbunge watasema ata-*swear allegiance*. Wakati mwingine tukija humu ndani tunajisahau sana, tunasahau kwamba waliotutuma ni Watanzania. Pengine hiki kifungu kwa Wabunge wapya wanaokuja ambacho kinasema mimi fulani kwa heshima kubwa ninaahidi mbele ya

Bunge Tukufu kuwa nitakuwa mtiifu na mwaminifu kwa nchi yangu Tanzania na kwamba naahidi kuilinda.

Mheshimiwa Spika, nadhani hiki ni kifungu kipya ambacho kitakuwa kinamkumbusha Mbunge husika kwa nini yuko humu ndani. Sisi uwepo wetu hapa ndani sio vyama vyetu, vyama vimetuleta, lakini tunavyofika pale mlangoni cha kwanza tunapaswa kuitanguliza mama Tanzania kama nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani hiki ni kifungu kipya kinacholeta uzalendo kitakachoisaidia sasa Bunge linalokuja kuweza kusimamia miiko ambayo tayari ameshaiahidi, kwa hiyo nipongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye kifungu ambacho Wabunge wengi waliotangulia wamekiongelea, utambulisho wa wageni Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, ninyi wote ni mashahidi, tumekuwa na changamoto ya muda humu ndani, ninyi wote ni mashahidi. Wakati mwingine tunakuwa na hoja ambayo mtu ulipaswa upewe hata dakika 15 unapewa dakika tano tu na sababu za msingi ni za muda, lakini unatambulisha. Hili ni eneo la umma, hii ni *public place* watu wanapaswa kuja wengi wanavyostahili. Hebu, niambie kila Mbunge akileta mgeni hapa tukafanya kazi ya kutambulisha, tutachangia humu Bungeni au tutafanya kazi ya kutambulisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili watu wanapaswa kuwa na *access* ya Bunge, utaratibu wa watu kuandika barua kuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo wakija kwa ajili ya mafunzo hizo ni *official trip* wana-*deserve recognition* na hiyo ni *group,* lakini wanapokuja mtu mmoja mmoja *sometimes* tunachukua muda mwingi kutambulisha.

Mheshimiwa Spika, nina *experience* ya Mabunge wengine, tumepata fursa Wabunge tofauti tofauti kutembelea Mabunge mengine duniani. Kama mmenda kwa *official trip* mtatambulishwa, lakini huwezi kufika, umefika pale Nairobi

umeamua kuingia Bungeni kuangalia shughuli za Bunge ukaamua kutambulishwa, haiwezekani. Mimi ninashauri kwamba kutengenezwe utaratibu na watu wajulishwe.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri nashukuru nilipata nafasi ya kutembelea Bunge la Uingereza. Watu wanaenda wanajiandikisha anakuja kama mgeni yaani ni wageni wa Bunge. Mtu yeyote ametoka mjini ninataka leo nasikia Anatropia anachangia naenda kumwangalia, sihitaji chochote zaidi kwenda getini kujiandikisha, nimevaa vizuri, niko salama niingie Bungeni nimwangalie Mbunge wangu anachangia. Nadhani na sisi tutengeneze hayo mazingira na je, iwapo kila mtu akiingia humu ndani tumtambulishe ni sawa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba mnikubalie mimi pia ni Mjumbe wa Kanuni mtukubalie kwamba tu-*save* muda lakini kama kuna *special purposes* mtu amekuja Bungeni tumtambulishe. Mimi wakati mwingine naona kama Bunge tumelitumia kama kutafuta *brand*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mtu ana ka-*NGO* kake amekatengeneza *portfolio* haijakamilika anakuja Bungeni unamtambulisha na anachukua ka-*clip* anatembea nako mtaani, nilikuja Bungeni mimi ni XX wakati ni ka-kampuni ka-kishikaji ni kitu hakijakaa vizuri tunampa *recognition* wakati mwingine ambazo sisi hatujazifanyia *vetting,* tunatumika sisi ku-*brand* vitu ambavyo haviko sawa. Kwa hiyo, mimi niwaombe kama kweli kuna *special mission* mtu mnapaswa kuja Bungeni atakuwa *vetted,* atakuja Bungeni atatambulishwa *that is a special mission.*

Mheshimiwa Spika, lakini wengine wananchi waruhusiwe kutembelea Bunge, wakaguliwe nje waingie watoke waingie watoke hili ni eneo lao ni Bunge la Wananchi wa Tanzania waingie Bungeni au wahitaji kutambulishwa na yeyote waone shughuli za Bunge waondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyingine ni kuhusu kura ya ku-*abstain.* Hii kura yaku-*abstain* kuna kambi yetu sisi huwa wakati mwingine tunapiga hiyo kura na hii niseme Mheshimiwa Spika nikupongeze

pamoja na Kamati husika kuiona kwamba ni ya msingi, wakati mwingine ukiipiga watu wanakuangalia sasa wewe uko wapi? Ni kura za kawaida ziko duniani kwamba mimi sijafanya maamuzi bado naendelea kutafakari. Kwa hiyo, kama sijafanya maamuzi siwezi kusema ndiyo au hapana, kwa hiyo, maamuzi yangu yatakuja siku nitakavyoamua kufanya maamuzi, kwa hiyo nayo niipongeze.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni mkutano wa Spika na Wabunge wote. Hiki kitu umeshaanza kukifanya na nikupongeze pia na Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe sisi tumekuwa na *forum* za kukutana na Mheshimiwa Spika wakati mwingine na Waziri Mkuu, zile *forum* wakati mwingine hatuzitumii vizuri. Unaenda unakutana na Mheshimiwa Spika badala ya kuongelea changamoto zinazowakuta Wabunge na Spika ndiyo pale unasema unajua tuna changamoto ya kahawa, tuna changamoto ya barabara, tuna changamoto ya nini.

Mheshimiwa Spika, lazima tujue kila kikao kina *forum* yake hii *forum* ya kukutana na Mheshimiwa Spika itakuwa inaongelea masuala ya Wabunge na Mheshimiwa Spika hii ninaiunga mkono naamini Wabunge wanaokuja wakitumia vizuri itafanya vizuri itakuwa na manufaa. Tunavyokua na changamoto ya *issue* za Bima ya Afya ninyi wote mnajua, Wabunge wamekuwa na Bima za Afya ambazo haziwezi ku-*cover* wazazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wamekuwa na Bima za Afya wengine hawajabahatika kupata watoto, lakini bima yake inaweza isiweze kum-*cover* mtu mwingine. Hayo ndiyo masuala, mkikutana na kiongozi wenu Mheshimiwa Spika mnajadili mnamwambia kwa sababu *specifically* inawahusu Wabunge na masuala mengine kadha wa kadha, nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Naoh Lemburis Saputu, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Musukuma ajiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hizi Kanuni ambazo zinahitaji kurekebishwa au kuwekwa sawa.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaanza pia na eneo la kutangaza wageni, nakubaliana na Kamati ya mapendekezo yake kwamba hili Bunge ni Bunge la wananchi na wapaswa kusikiliza ndani na nje. Kwa misingi hiyo, ni vizuri wakaingia wanapotaka hata kama wasipotambulishwa lakini wakaingia ili pia hili Bunge wakati mwingine unakuta muongoza kikao kama ni Mheshimiwa Spika au ni Mwenyekiti analazimika kukatisha shughuli halafu anatambulisha wageni karibu mara tatu, hiyo nayo ni sehemu kidogo ambayo ukiunganisha inakuja kutuletea ukosefu wa uchangiaji, unakuta mtu anachangia dakika tano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili tuliangalie lakini tunapoangalia kuingiza wageni ni vizuri sasa twende tuangalie pia eneo la uchangiaji.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine Mbunge anasimama anachangia dakika tano, sasa dakika tano kuchangia ni ndogo sana kwa Mbunge hasa ukizingatia kwamba kuna mawanda mapana ya kuhakikisha kwamba unaeleza mambo ya wananchi. Kwa hiyo, hata wakati ule ilipopunguzwa dakika kumi na tano naona ilikuwa ni busara, lakini sasa inaonekana kuna umuhimu wa kuangalia tena huu muda wa uchangiaji. Hiyo inaenda sambamba na kuangalia namna ya kuwatambulisha wageni katika mapendekezo ya Kamati…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa…

**SPIKA:** Mheshimiwa tena na hicho kifungu cha Taarifa nadhani kinafanyiwa marekebisho, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Mheshimiwa Noah anaongea vizuri kwa kweli unakuta Mbunge amepewa labda dakika kumi, katika zile dakika kumi zake wanasimama watu watatu tofauti wakitoa taarifa. Sasa katika zile taarifa zinachukua hata dakika moja au mbili au tatu zinahesabika kwenye dakika kumi ambazo amepewa Mbunge. Kwa hiyo katika vile anavyoongea nilikuwa nataka niboreshe tu na nashukuru umesema hicho kipengele kipo kama kipo kama taarifa inatolewa iwe ya zile dakika kumi au dakika tano au saba ambazo amepewa Mbunge. Wanatoa taarifa dakika zao zihesabike kama ni za taarifa na Mbunge dakika alizopewa kama ni kumi zibaki kumi zilezile. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa ya Mheshimiwa Esther, sasa ndiyo hicho nachosema kwamba tuangalie kwa sababu wakati mwingine huu muda wa kuchangia ni mdogo sana, sasa mtu anavyokupiga taarifa anachukua kama dakika mbili tatu hiyo nayo ni changamoto nyingine unakuta ulikuwa na *point* za kumalizia inashindikana. Kwa hiyo hili nalo tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, lakini nije kwenye eneo la mavazi; kwamba mavazi rasmi ya Bunge yanaeleweka, suti ni rasmi hata hii niliyovaa hapa ni rasmi. Kwa hiyo, sasa changamoto inakuja pale ambapo kuna watu wengine ambao siwezi kutaja wanavaa katika mazingira yaani sijajua hapa Bungeni lazima kila mtu anatakiwa ajiheshimu kwa kadri ambavyo amelelewa na wazazi wake, ndugu, jamaa na marafiki, familia aliyotoka na tamaduni. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kwamba sisi Wabunge tunapoingia Bungeni tumevaa vizuri ili kuweza kuweka unadhifu na heshima ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, mimi nina jambo lingine kwenye eneo la Taarifa ya *CAG*. Taarifa ya *CAG* inawasilishwa mwezi wa tatu,

halafu tunakuja kujadili mwezi wa kumi na moja, kidogo hii inaleta ukakasi kwa wananchi kwamba Bunge wao wanakuja kujadili taarifa wakati imeishapoa. Sasa hili nalo ebu tuliangalie namna ya kufanya kwa sababu nadhani ulifanya marekebisho kwa maana ya kusaidia Bunge wakati ule, lakini sasa naona bado kuna *gape* hapa karibu la miezi karibu mwaka mzima hii nayo taarifa hii tuingalie kama tunaweza tukaiwahi ikishawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais, ikiwasilishwa Bungeni basi tuangalie namna hii huu mjadala ufuatane ili tumalizane na hilo hiyo *gape* ya kujadili taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo tulitakiwa tuliangalie ambalo la msingi sana la muhimu suala la bima kwa Wabunge kama sasa bima unayo Mbunge na haimsadii mzazi wako, haimsadii mama yako, haimsadii baba yako, kwa kweli hili nalo wakati kwenye kada zingine unakuta mtu ana-*cover* watoto na wazazi lakini ikija kwa Mbunge hawezi ku-*cover* wazazi kidogo hii Mheshimiwa Spika ebu tuliangalie tena kwa sababu siyo vizuri haiko vizuri. Kwa sababu kama unaamua kutoa huduma kwa familia ile basi itolewe kama ambavyo inatolewa pia kwenye kada zingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nikupongeze sana pia kwa jinsi unavyoongoza Bunge letu pamoja na mapungufu mbalimbali yaliopo kwenye Kanuni zetu lakini umekuwa ukijitahidi sana sana sana na Mwenyezi Mungu akubariki sana kwa uwezo wako huo na nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima James Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Tarimba Abbas ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mimi nitazungumza kwa ufupi. Kwanza nakubaliana na hoja ya wageni Bungeni imeshaelezwa kwa kina na waliotangulia kwamba Bunge lina muda mdogo sana wa kujadili mambo mbalimbali ambayo ni muhimu kwa maslahi ya Taifa. Kwa hiyo, nadhani Kamati ya Kanuni imetumia busara kubwa sana kuonesha wazi kwamba ni wageni wa namna gani watambulishwe kwa umuhimu wake, kwa

hiyo ni eneo ambalo nadhani ni muhmu sana tukalikubali kama Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina eneo dogo ambalo sijaona kama likuwa *covered,* bahati mbaya hatujapata hizi Kanuni in *advance*. Kwa hiyo, nime-*relay most* na hotuba ambayo imesomwa na Mheshimiwa Naibu Spika kwenye eneo la ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo ya *CAG* na maagizo ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge ambao tumepewa dhamana ya kuwa Wajumbe wa Kamati ama za *PAC* ama za *LAAC* ambazo tunafanyakazi kwa niaba ya Bunge kwa mantiki ya kwamba tunafanyia kazi Taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo amekuwa amezileta. Sasa majukumu yetu sisi ni kusimamia fedha za umma na kuangalia kama matumizi ambayo Bunge limeidhinisha yamefanyika na yamefanyika kwa ufanisi na mkaguzi amekagua amejiridhisha na kama kuna changamoto ambazo zinahusiana na Wizara, Idara na Halmashauri zetu *then* wanatakiwa wafanye marekebisho ili basi matumizi ya fedha yaendane kiutaratibu.

Mheshimiwa Spika, sasa nakumbuka wewe kwa busara zako mwaka jana mwezi wa sita baada ya Bunge kupitia Kamati zetu kutoa taarifa zake na kutoa Maazimio ya Bunge ambayo Serikali wanatakiwa wayatekeleze, wewe kwa busara zako ukaanzisha *session* ambayo tutakuwa sasa tunafuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yalivyotekelezwa na upande wa Serikali kutokana na ripoti hizi za *CAG,* sasa hiyo ilikuwa ni busara yako.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tunaamini kwamba kwa ajili ya kutengeneza uwajibikaji ni muhimu kanuni zetu zikaainisha kwamba pale ambapo Bunge linaazimia tusisubiri tena mpaka mwaka mwingine ambapo Kamati husika zinatoa ripoti ndani ya Bunge ndiyo tuanze kuelezewa utekelezaji ulikuwaje. Ili kutoa wajibu kwa Serikali ama kila baada ya miezi mitatu ama kila baada ya mwezi baada ya taarifa kusomwa, Maazimio ya Bunge kusomwa juu ya utekelezaji wa Taarifa za *CAG* watuambie wametekeleza nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma taarifa hizi hii tu ya Mkaguzi wa juzi inaonesha kwamba kwa mapendekezo ambayo tuliyotoa ya mwaka uliopita yametekelezwa kwa 35% tu, 35% tu. Kwa taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuna mapendekezo tokea mwaka 2019 hayajatekelezwa, mwaka 2020 hayajatekelezwa, mwaka 2030 hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu watu wanajua kwamba hawana kipindi ambacho wanatakiwa waje walieleze Bunge kile ambacho tumewaambia wakanyie marekebisho wamefanyia kiasi gani wana-*relax*. Sasa tukitengeneza hiyo ratiba maana yake Mawaziri waliopewa dhamana kuwasimamia ma-*accounting officer* huko watahakikisha wanakimbizana nao ili hizi hoja zifike mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni suala la aibu, kuna hoja zina miaka kumi hazijajibiwa, kuna hoja zina miaka mitano hazijajibiwa lakini watu wapo tuu hakuna kuwajibishana. Sasa mimi nilidhani, nilidhani ile busara yako kubwa sana mwalimu wangu mimi makini, ehee huyu ni mwalimu wangu na hiki kichwa ukikiona ujue kilikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulitumia busara ambayo waliokutangulia hawakuitumia na ambayo tunapoenda huko kwenye Mabunge ya wengine, kwenye vikao hivi vya Kamati za *PAC, LAAC,* Kamati za *oversight* Afrika tunajisifia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kuna wengine huko bado wanazurura, tunasema *no* sisi tumeanza kutembea kwamba tumekuwa na kipindi ambacho Spika wetu ameendelea kusema Serikali mje mtoe ripoti hapa ili tuwajibike, kama Waziri umepewa dhamana unashindwa kusimamia watu wako tule kichwa, kama Mkurugenzi amepewa dhamana anashindwa kusimamia pesa aliwe kichwa, bila hivyo tunakuwa Bunge la kulalamika tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkaguzi anaonesha mambo, anaonesha matumizi mabovu ya pesa, yanaonesha ukiukwaji wa Sheria za Fedha tunalalamika tu. Sasa tuweke sindano pale tukipiga ile *pin*

vizuri hawa majamaa hawatakuwa na dharau sasa hivi hawapo wako wapi? Yaani tunajadili mambo muhimu Serikali haipo. Kwa sababu wanatuona sisi ni Wabunge wa kulia lia wakati sisi Wabunge tumeteuliwa na wananchi kuja kusimamia pesa za umma zinavyotumika kwa uadilifu kwa manufaa ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba kwa ruska yako naomba hili jambo liweze kuingizwa kama halipo kama lipo ninalibariki, lakini sijapata muda wa kupitia na sijamsikia Mheshimiwa Naibu Spika akiliwasilisha, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Abbas Tarimba na Mheshimiwa Ally Kassinge ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia mabadiliko ya Kanuni kwanza nikushukuru kwa kipindi chako cha miaka mitano umekuwa Spika wa kiwango sana.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mabadiliko haya tusiende kuchafua taswira ya Bunge letu. Mimi ni Mbunge wa awamu ya pili naenda ya tatu na kama mipango ya Mungu tutakuwa hai mimi ninauhakika wa kurudi kwa sababu nimeishafanya tathmini yangu awamu ijayo ndiyo nilitegemea nianze kuwaalika wageni mimi sijawahi kualika mgeni hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 165 inasema kifungu cha kwanza na pili imeeleza watu watakaotambulishwa humu Bungeni, naona kama tunaenda kufanya ubaguzi, kwa sababu hawa watu waliotajwa kutambulishwa Spika anaweza akamtambulisha yeyote ambaye ameona amefanya kitu kikubwa kwenye nchi yake, yeyote awe msanii, awe mwanariadha, mtu yeyote aliyefanya jambo kubwa kwenye taifa. Sasa tunapokuja humu ndani sisi Wabunge kuwaalika watu kuja Bungeni ni moja ya ahadi tunazozitoa wakati tunatafuta kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa jiulize kilometa zaidi ya 900 unamtoa mtu Geita huko unamleta Bungeni anapata baridi hapa na Sumbawanga huko mbali, anapigwa baridi hapa halafu anamaliza anaondoka tu kama *group* la mbuzi, hapana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nadhani tulivyokuwa zamani tuendelee vilevile. Kama ni suala la muda kama alivyoeleza mtoa hoja Naibu Spika kama ni suala muda humu ndani Bungeni tuna *canteen* tunatoka saa saba na humu tuna madaktari wa binadamu muda wa kupumzika binadamu unaanza saa nane baada ya kula ndiyo mtu anaenda kupumzika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushauri kama suala ni muda tusogeze kutoka saa saba twende saa nane kwa sababu humu ndani tuna muda wa chai, tuna *canteen* tunaruhusiwa, tuna chakula. Mtu utaenda saa nane tufunge halafu tukapumzike masaa mawili tunatoka humu saa saba unalala kuanzia saa nane, saa tisa, saa kumi tunarudi saa kumi na moja…

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa…

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Francis Mtinga.

**TAARIFA**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anazungumza vizuri sana, naomba tu nimpe taarifa kama ni suala la muda badala ya saa nane tunaweza tukarudi hata saa kumi badala ya saa kumi na moja. Nakukupa taarifa ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naipokea.

Kwa hiyo, kwa heshima kubwa ya Bunge hili sisi tumelikuta Bunge hili lina hizi Kanuni tunaenda tunabadilisha, lakini nilikuwa naomba sana ushauri wangu kwenye hili tuendelee na utaratibu

wa kutambulisha wageni wetu, kwanza ni heshima. Unaleta wageni watano kutoka jimboni kwako kwa sababu yeye hawezi kuwa Mbunge, lakini alikupigia kura, Watanzania na wanajimbo wenzie wakimuona alialikwa, ametambuliswa naye ameniga katai kama Kasalali inampa heshima hata kwenye jamii kule kwamba anatambuliwa na Mbunge wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa nashauri sana kama suala letu ni muda, kama tatizo ni muda kwamba tunabanwa muda tutoke saa saba tuondoke Bungeni saa nane, mtu anayepata njaa unaenda *canteen* unarudi muda wa saa moja utaendelea kutupa huduma ya kutambulisha wageni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine sikuliona lakini naomba nishauri, sisi humu ndani siyo wahuni ni Waheshimiwa tuna familia kama jinsia ya kike ana mume wake, wa kiume ana mke. Sisi tumepewa heshima ya kupita *VIP,* lakini nataka kujiuliza ukienda pale *VIP* mkishuka kwenye gari kama huna hela inabidi mgawanyike, mwanamke apite huku wewe upite huku na sisi ili upate kura lazima kuna mume nyuma kuna mke nyuma yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sioni kama wenzetu walitengeneza utaratibu mzuri na sijui kwa nini? Kwa sababu ni Bunge nilikuwa nashauri ile heshima ya *VIP* hasa kwenye hizi sehemu tunazopita ni mbaya sana kumtengenesha mtu na mwenza wake. Kwa sababu pengine tunafinya nini mimi sielewi, sisi tumefunga ndoa tumeambiwa mtakuwa mwili mmoja tukifika kwenye *VIP* tunakuwa miili miwili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri sana kwamba hii heshima tuliyopewa ya *VIP* iende kote kwa mtu aliye na mwenza wake ambaye hana mwenza atapita peke yake, kunitenganisha mimi na mkewangu tunakuwa pia tunakiuka maadili ya ndoa ambayo mimi nimeapa kuyalinda kama nilivyoapa kuapa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la muda, kwenye Kanuni inasema tutachangia kwa dakika kumi, lakini kwa uzoefu

tumeona mara nyingi ukichangia tu zikifika saba sasa sijajua kakengele huwa kako wapi? Kanalia *kriii* saa nyingine hata tano tu sasa sijaelewa labda kama umetoka kwenye maada kanabonyweza.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri kwa sababu Kanuni imetaja dakika kumi anayekaa kwenye kiti anajua dakika kumi zangu nitazigawa kwa watu sita siyo lazima wote tuongee. Kiukweli muda wa kuchangia ndiyo muda hasa wa kueleza matatizo ya wananchi wetu, unapochangia dakika tano unajitambulisha na kumpongeza Spika kengele imelia. Kwa hiyo wale waliofikilia dakika kumi mpaka kumi na tano ninadhani tungeendelea kuziacha zibaki pale. Wale ambao watakosa nafasi siku ile wachangie siku inayofuata.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ninakupongeza sana na kukutakia kila la kheri kwa jinsi unavyotuongoza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimba Abbas, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Kassinge. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu sana. Mimi nina maeneo mawili ambayo ningependa kuchangia.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni upande wa kuanzisha kiapo cha uzalendo, ni jambo jema sana na litatusaidia sisi Wabunge kujielekeza katika yale mambo ya kimsingi na hakika kipindi chote tutakapokuwa Wabunge tuweze kuonekana kweli Mbunge fulani ni mzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa eneo hii linahitaji mimi kwa mapendekezo yangu tungetengeneza *standards* fulani ambazo kwazo mtu anaweza akapimiwa nazo kwamba ukifanya mambo kadhaa basi wewe kweli umetimiza kiapo chako cha uzalendo, lakini ukienda kinyume na mambo fulani ambayo yanaweza

yakatajwa basi kipimo kile kitaonesha kama kweli wewe umekosa uzalendo.

Mheshimiwa Spika, ningependa twende mbali zaidi pale ambapo Mbunge ataonekana amekosa uzalendo nini kinachofuata, kwa sababu tusiseme tu kwamba kuna kiapo cha uzalendo na kama mnavyojua kuna watu wengine wanakwambia uzalendo umetushinda. Tunayasikia hayo katika michezo hasa. Sisi tungependa tujiongoze vizuri zaidi, Wabunge wa Bunge la Tanzania hakika wakati wote pamoja na utii wa Katiba, lakini utii wa kizalendo ni jambo muhimu sana. Niwapongeze wale ambao walifikiria kuliongeza hili katika kanuni zetu. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona, nilikuwa nina taarifa kidogo fupi kwa Mbunge makini Mheshimiwa Abbas Tarimba kwamba tumeongeza kiapo cha pili cha uzalendo na tupo na kiapo cha utii kwa Katiba ya nchi.

Sasa ni vizuri kanuni zetu ziweke bayana kwamba, ni wakati gani Mbunge atakuwa amekiuka chochote katika viapo vyote viwili na adhabu yake iwe nini katika kipindi cha uhai wa Bunge. Maana kuwa na viapo tu ni jambo moja, lakini kusimamiwa kwa viapo ni jambo muhimu zaidi, vinginevyo tutakuwa na viapo vizuri lakini hakuna ufuatiliaji juu ya viapo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninashauri ninampa Taarifa rafiki yangu kwamba ni vizuri hivyo na Kamati ya Haki ipate nafasi ya kushughulika na kuleta mapendekezo kwa Bunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea kwa mikono miwili. Nimshukuru sana Mheshimiwa kwa kunipatia taarifa ambayo hakika ndio ilikuwa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, jambo langu la pili ni juu ya kupeperusha bendera za Wabunge. Kuna Wabunge ambao tunatoka katika mikoa ambayo hatuwezi tukapeperusha bendera kwa mfano, Wabunge tunaotoka Dar es Salam. Ninaamini hata tukiwepo Dodoma hatupeperushi bendera na tukienda Zanzibar hatuwezi tukapeperusha bendera.

Mheshimiwa Spika, sasa inatokea wakati kuna misafara ya kitaifa, hata misafara ya kimkoa ambapo tunatakiwa tufike maeneo fulani kwa haraka ama saa nyingine tunakuwepo katika ile misafara, lakini magari yetu kwa kuwa hayana utambulisho wowote ule, kwa mfano, mimi ninajizungumzia sisi ambao tunatoka Dar es Salaam magari yetu hayana utambulisho wa aina yoyote, hatuwezi tukapeperusha bendera. Tunajikuta katika ile orodha ya watu ambao wamo katika msafara labda pengine gari lako linawekwa nyuma kiasi kwamba wanaofikia pale mbele hata ukiitwa Mbunge njoo utoe salamu, ndio kwanza unatafuta sehemu ya ku-*park*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa ninafikiria kama kanuni ya kupeperusha bendera inaweza ikaendelea, je, Bunge haliwezi likafikiria kwamba labda tunaweza tukawa na *number plates,* kwa mfano, mtu unachagua gari lako moja ambalo ungelitumia kwenye shughuli zako za kikazi likawa na *number plate* ambayo inaashiria kwamba gari hili ni la Mbunge ili kuweza kumsaidia pale mahali ambalpo anatakiwa afike haraka *either* barabarani ukikutana na *traffic* ukajieleza bwana mimi ninawahi mahali fulani, ama ukiwepo katika misafara ili na wewe usiweze ukaharibu *protocol* za misafara ukawa unawahi na gari yako ikapewa heshima ya kuwepo pale, ili uweze kutekeleza wajibu wako wa Kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na mawazo hayo mawili na ninaunga mkono hii hoja iliyopo mbele yetu na ninashauri marekebisho kama haya pia yaweze kuingizwa. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ajiandae.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi hii ili na mimi nipate fursa ya kuweza kuchangia hoja ya Kamati yetu ya Kanuni ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, asubuhi ya leo mchango wangu utajikita katika maeneo makubwa mawili; eneo la kwanza ni eneo la mavazi na eneo la pili itakuwa ni ile kanuni inayohusu masuala ya taarifa wakati mjadala hapa Bungeni unaendelea.

Mheshimiwa Spika, nikianzia na mavazi kwanza na mimi niungane na wachangiaji ambao wanaamini katika mavazi ya kimila. Niseme tu kwamba ni vizuri sasa kanuni hizi zikaweka wazi kwamba haya mavazi ya kimila yawe yanaratibiwa kwa namna ipi kiasi ambacho isiathiri masuala ya mila husika pia mila za kinchi na pia isiathiri taratibu za uendeshaji wa Bunge letu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mavazi maarufu ya kimila katika nchi yetu ni ya ndugu zangu Wamasai kaka yangu Ole-Sendeka pale. Ni mavazi ambayo Watanzania wengi tumeyaamini na tukayakubali kwamba ni sehemu ya mavazi yetu ya kimila. Ifikie mahali Bunge letu liwe linatambua mavazi kama haya na Mbunge akivaa mavazi kama haya akija Bungeni iwe ni sehemu ya mavazi rasmi yanayotambulika ilimradi tu kwamba yasiendane na vile vikorombwezo nitumie lugha hii ambavyo…

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ana hoja kwenye hiyo Taarifa ambayo unataka kumpa, anataka kusema kwenye kanuni. Haya Mheshimiwa Kassinge kuna taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kuendelea na umakini wako wa kutuona. Mimi ninataka kumpatia Mbunge makini Mheshimiwa Kassinge taarifa kidogo kuhusu mavazi haya yanayotambulisha asili yetu.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la busara sana pale ambapo si tu wageni waendelee kuruhusiwa kuja ndani ya Bunge wakiwa wamevaa mavazi ya asili na hasa haya ambayo wenzetu mpaka kwenye Mashirika ya *UN* wameyakubali mavazi kama haya ya Wamasai na wengine, lakini pia hata ikiwezekana ndani ya Bunge la Jamhuri la Muungano siku mojamoja mnaweza mkaturuhusu tukaingia katika mavazi ya asili katika siku moja ndani ya siku tano za kazi, tuingie na mavazi ya asili. Nilitaka nimpe taarifa tu. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma ninaomba uketi kidogo kwa sababu Mheshimiwa Ole-Sendeka alikuwa anatoa taarifa kwa Mheshimiwa Kassinge. Sasa naona umesimama kumpa yeye taarifa. Sasa ngoja Mheshimiwa tumalize kwanza taarifa aliyokuwa anapewa Mheshimiwa Kassinge. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Kassinge, Taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa hii ninaipokea na nikihitimisha eneo dogo hilo la mchango wangu ni kwamba ilimradi tu mavazi haya yawe yanaratibiwa katika namna ambayo haitaathiri masuala mengine. Kwa mfano,…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ya Mjumbe, lakini wasiwasi wangu kwamba mavazi yetu ya mila mengine yana *attachment* mpaka uwe na kitu fulani ndio likamilike, kama la ndugu yangu Sendeka mpaka na kisu. Sasa itakuwaje? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea taarifa hii na ndio nilikuwa ninataka nihitimishe hivyo kwamba ili mradi tu mavazi haya yasiendane na vingine vinavyoongeza katika vazi hilo ambavyo pengine kitaratibu zetu za kiusalama haikubaliki. Kwa mfano, kuwa na kisu au sime au hata rungu ninadhani kidogo inakuwa si sawasawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo la mavazi nizungumzie pia mavazi ambayo Wabunge wanapaswa kuvaa wanapokuwa katika shughuli zetu za Kamati. Kumekuwa na tofauti kidogo kwamba tunapokuwa katika mijadala kwenye jengo hili hapa kwenye huu ukumbi, mavazi ambayo tunavaa ni haya kwa asilimia kubwa kwa wanaume ni suti za namna mbalimbali na kwa kinamama ni mavazi nadhifu.

Mheshimiwa Spika, lakini tunapokuwa kwenye shughuli za kamati imekuwa ni tofauti kidogo kwamba kwa kina baba suala la suti halijawekewa mkazo badala yake imezungumza mavazi nadhifu. Sasa hofu yangu pia kwa mujibu wa uzoefu uliopo ni kwamba, kwneye Kamati inatokea baadhi ya Wabunge wanavaa yale ambayo katika haiba ya Kibunge kidogo mimi kwa maoni yangu ninaona si sawa. Kama vile mtu anavaa labda *jeans*, *t-shirt,* kidogo ninaona si sawa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninashauri kwamba kwa nini mavazi ya Wabunge katika Kamati…

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Kassinge kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe. *(Makofi/Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, kaka yangu anachangia vizuri sana kwamba wakati wa shughuli za Kamati kuna suala la ukaguzi wa miradi. Sasa ukitaka kwenye Kamati twende tukakague miradi tumevaa suti ninadhani pia haitapendeza. Ni vizuri ikawa tu mavazi nadhifu ambayo yanatunza heshima ya Bunge lakini isiwe sasa twende na tai tunakwenda kukagua maboma jamani! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea taarifa hii katika misingi tu kwamba Kamati zimegawanyika katika maeneo makubwa mawili; kuna kamati za kukaa mezani na tuna wageni ambao tunawaita wataalamu wa Serikali. Sasa inapotokea katika mazingira ya shughuli za mezani za Kamati halafu Mbunge upo na *t-shirt,* Afisa wa Serikali amevaa suti nadhifu kidogo naona inapunguza hadhi ya Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa taratibu zile sasa za ukaguzi wa miradi hilo ni jambo ambalo halina shaka sana japo kwamba sita-*entertain* sana kusema watu wavae *jeans* kwenye ukaguzi wa miradi ibaki tu kwamba wavae mavazi nadhifu ambayo hata mtu wa kawaida akimuona anajua huyu ni Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo langu la pili la mchango wangu ni eneo la kanuni ile inayohusiana na taarifa. Msingi wa kipengele hiki cha taarifa ni ama kuongeza thamani au mchango kwa mchangiaji ambaye anaendelea kuchangia. Kwa mfano ambao umetokea hivi punde, mchango ambao nilikuwa ninachangia mimi Mheshimiwa Ole-Sendeka akawa ameongeza thamani, Mheshimiwa Saashisha ameongeza thamani, Mheshimiwa

Musukuma ameongeza thamani. Hii ni maana halisi ya taarifa katika uchangiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili mantiki ya taarifa ni pale ambapo pengine Mbunge hana uelewa wa kutosha na kile ambacho anakizungumza au anakusudia kupotosha kwa kujua au kwa kutokujua na kwa maana hiyo sasa taarifa inatolewa, ili kunyoosha kile ambacho pengine kingepotoshwa badala yake ukweli ukoje.

Mheshimiwa Spika, sasa, kama tutajikita katika maeneo hayo mawili kwa maana ya kuongeza thamani ya mchango au kukosoa na kurekebisha, nadhani eneo la taarifa hili halina shida yoyote. Sasa *practice* iliyopo ni kwamba baadhi ya Wabunge wamekuwa wakitoa taarifa kana kwamba anapata na yeye *forum* ya kuchangia yale ambayo anadhani achangie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo ndipo ambapo mimi binafsi ninaona dhana ya taarifa kidogo tunaipotosha. Kwa maana hiyo, kama tutajikita katika maeneo yetu yale ya kuongeza thamani ya mchango au kurekebisha kile ambacho kinapotoshwa, mimi sioni sababu ya muda wa mzungumzaji kuongezwa. Utabaki ule ule kwa sababu itakuwa inaongeza sehemu ya mchango wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na pia ninaomba kuunga mkono hoja ya Kamati yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile. Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji ajiandae.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi hii na awali ya yote nikupongeze kwa kazi nzuri unayoendelea kufanya, lakini zaidi kwa tamasha kubwa ulilolifanya kule Uyole wakati wa kutanganza nia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikutakie kila la kheri kwenye safari mpya ambayo inaenda kuanza muda si mrefu ujao na niwatakie kheri

Wabunge wenzangu tunapoenda kwenye mchakato muhimu kisiasa unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sikuwepo wakati Mheshimiwa Naibu Spika akiwasilisha, lakini nimekuwepo wakati akichangia jirani yangu hapa Ole Saputu pia na Mheshimiwa Ole-Mdee kuhusiana na mambo ya *oversight* (uwajibikaji).

**MBUNGE FULANI:** Ole-Mdee?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nijue kama mnanisikiliza. Mheshimiwa Mdee. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la *oversight* na Bunge kama chombo kikuu na muhimu kwenye Taifa letu cha uwajibikaji nilikuwa nina maoni mawili ama matatu yafuatayo katika kuboresha na ninadhani uboreshaji ungepaswa kutokea kuanzia kwenye eneo la Katiba, lakini kwa sababu hatujadili Katiba ninadhani kuna machache tunaweza tukayafanya katika *level* ya kanuni zetu za Bunge. Kwa hiyo, ninaomba kama ni mchango muafaka basi nyongeza hii iwekwe kwenye mjadala wa kanuni mpya ambazo zitaenda kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu yanaanza na *quote* aliyoitoa mwaka 1887 Lord Acton yaani John Dalberg Acton, ambaye alisema kwamba; "*Power tends to corrupt and absolute power corrupts absolutely. Great men are almost always bad men.*"

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri sisisi isiyo rasmi ni kwamba; madaraka huwa yanalevya ama huwa yanapotosha, lakini pia madarakia makubwa sana huwa yanalevya zaidi. Pia watu wazuri na watu mashuhuri huwa wakati mwingine wanakuwa ndio watu wabaya zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mifumo ya uongozi na usimamizi wa mataifa kuna mihimili mitatu; kuna mhimili wa *Executive* (Serikali Tendaji), pia mhimili wa Mahakama na Bunge. Sasa hii mihimili inafanya kazi kwa kutegemeana na ni ngumu

sana kusema unaweza ukachora mstari ambao unaweka mipaka kati ya utendaji wa mhimili mmoja kwenda mwingine, inaingiliana. Kwa hiyo, *separation of power is not absolute*.

Mheshimiwa Spika, sasa, kwa msingi huo mhimili wa Bunge unapaswa kwa namna yoyote ile kuusimamia kwa ukaribu na kwa wivu mkubwa sana mhimili wa *Executive* kwa maana ya mhilimili wa Serikali Tendaji. Kama kukiwa hakuna usimamizi madhubuti itakuja ule msemo anaosema Lord Acton kwamba, *absolute power* ina-*corrupt absolutely.* Sasa ili kuepuka hilo Taifa letu limeweka msingi wa uwajibikaji ambapo Bunge ndio chombo cha juu kabisa cha kuisimamia Serikali na imo kwenye Katiba ninafikiri ni Ibara ya 63(2) kitu kama hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika mfumo wetu wa uwajibikaji ambapo sisi kama Bunge ndio tunapaswa kuisimamia Serikali ipasavyo kuna changamoto nyingi ambazo nitazitaja kwa uchache wake kama ifuatavyo; ambazo ningependa kuona kanuni zitakazoenda kuboreshwa basi zinazingatia maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kwamba sisi tunategemea jicho la Serikali ambalo ni Ofisi ya *CAG* kutuletea taarifa za ukaguzi ambapo zinapitia kwa Mheshimiwa Rais ambaye naye kama sehemu ya Bunge anazileta kwetu tunazichambua kwenye zile Kamati zetu za *oversight,* halafu tunatoa mapendekezo kwa Bunge. Bunge linatoa maazimio kama alivyosema vizuri Mheshimiwa Halima Mdee.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana wakati mfumo huu wa uwajibikaji unaanza kufanya kazi, *CAG* anafanya *sampling* ya taasisi na mashirika ambayo ataenda kuyakagua, anakagua kwa uchache wake kwa sababu hawezi kukagua wote kwa wakati wote. Akishafanya *sampling* anatuleta yale yaliyojitokeza. Tunapofika na sisi kwenye Kamati kwa muda mchache tulionao na sisi tena tunafanya *sampling,* tunachukua tena machache ambayo tunaweza kuyakagua na tunaweza kuyatembelea.

Mheshimiwa Spika, halafu na sisi tena tunaleta Bungeni kutoka kwenye ripoti yetu kwenye zile Kamati zetu za *oversight, sample* tena ya taasisi kwenye mambo machache ambayo tumeona ni muhimu yakaja kujadiliwa na Bunge. Halafu kwenye Bunge watachangia Wabuge wachache ambao pia watapewa muda mchache, ambao na wao watachagua sehemu za kuchangia ambazo ni chache pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo yake mpaka tunafika mwisho wa ule mfumo ambapo sasa Bunge linatoa maazimio yake tayari tumesha-*dilute* sana mambo ambayo yalionekana kwenye ripoti ya awali ya *CAG* ambaye pia alikuwa amefanya *sampling*, siyo amefanya kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa lengo zima la kufanya ukaguzi na hatimaye kufanya mfumo wa usimamizi ufanye kazi linakuwa *defeated in a way,* halafu baadaye sasa ripoti ya utekelezaji inapokujakutolewa unakuta wametoa ripoti ya utekelezaji kwenye maeneo machache sana, na maeneo mengine hawajatekeleza hata kimoja kutoka katika yale Maazimio ya Bunge. Utapita mwaka mmoja, mwaka wa pili, mwaka wa tatu, hata miaka 10 mapendekezo yaliyotolewa na Bunge ama maazimio hayajawahi kufanyiwa kazi, maana yake ni kwamba ni kama vile tunatwanga maji kwenye kinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uwajibikaji na uwajibishaji wa watendaji kwenye Serikali hayaonekani moja kwa moja. Wananchi wamekuwa wakilalamikia sana jambo hili na Bunge linapaswa kufanya kazi yake kwa niaba ya wananchi ili sasa uwajibikaji uonekane na usimamizi wa mali za umma uonekane.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, nilidhani watakaoenda kuchambua hizi kanuni, pamoja na mapendekezo yaliyosomwa hapa na Mheshimiwa Naibu Spika watazame sana eneo la kuboresha mfumo wa uwajibikaji ambao unaanzia kule chini, ili basi kama inawezekana pengine muda wa sisi Kamati zile za..., watakaokuwa kwenye hizo Kamati za Usimamizi waweze kupata muda wa kutosha wa kufanya kazi kubwa ya uchambuzi wa taarifa za *CAG*. Hiyo ni katika hatua ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, pia katika hatua ya pili kuwe kuna muda maalum wa kusimamia kama yale mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge yakaletwa kwenye Bunge yakageuka kuwa maazimio yametekelezwa na yametekelezwa kwa kiasi gani, lakini pia itafutwe namna ya kuwawajibisha wale watendaji moja kwa moja na tupate ripoti ya uwajibishaji hapa kwenye Bunge. Tukifanya hivyo walau tutaanza kuona kwamba yale madaraka makubwa ambayo yako *vested* kwa watendaji kwenye *Executive Arm* ya *government* yanadhibitiwa, yanakuwa *checked*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu bila kuwa na *checks and balances* kwa hakika *absolute power* ambayo tumewapa mhimili mkubwa huu na muhimu wa *Executive* yata-*corrupt* mfumo wetu wa utendaji na usimamizi wa rasilimali za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, miaka ile ya Bunge la Mheshimiwa Mama Makinda mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati, tuliwahi kwenda kutembea kwenye Bunge la kule Uingereza. Kule tulikuta Kamati zile za *oversight* zinafanya kazi mwaka mzima. Kwa hiyo, wajumbe wale kutokana na umuhimu wake, wajumbe wanaokuwa kwenye zile Kamati wanapata fursa ya kwenda kufanya ukaguzi mwaka mzima. Kwa hiyo, ni mjumbe mwenyewe anaamua tu, ilimradi *quorum* iwe imefika, anaripoti mimi nitatoka siku hii mpaka siku hii sintokuwepo, lakini kuanzia siku hii mpaka siku hii nitaambatana na Kamati kwenda kwenye ukaguzi na usimamizi wa miradi, ama kwenye vikao vya uchambuzi wa taarifa anatokea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inakuwa hakuna ile *limit* ambayo inawekwa kwenye Kamati nyingine za kawaida za *Parliamentary Standing Committees* nyingine za kisekta ukilinganisha na mabunge mengine. Kwa hiyo, kama Mabunge ya *Commonwealth* na sisi tunafuata mfumo wa *Commonwealth*, wameweka mfumo huo kwa Kamati za *oversight*, ni ushauri wangu kwamba pengine tunhitaji kutazama suala la muda wa utendaji kazi wa hizi Kamati, lakini pia hata suala la wajumbe wanaoingia kwenye hizi Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama watakuwa idadi ni ile ile ndogo kama ilivyo sasa, kipindi ambacho Wabunge hawawezi kushiriki kwenye hizi Kamati maana yake tutakuwa tunapata shida ya *quorum*, lakini kama idadi ya Wajumbe pia itaongezeka, pengine labda Wenyeviti wa Kamati nyingine wakaingizwa kwenye hizi Kamati za *oversight* wakawa wanaingia *by virtual of their positions*, maana yake idadi ya wajumbe inaweza ikawa kubwa na tusipate shida ya *quorum*, kama zitakuwa zinafanya kazi kipindi cha mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata kama ikitokea Wajumbe wamekuwa wengi, maana yake wanaweza wakagawana kwenye maeneo mbalimbali wakashambulia taasisi zote ambazo zimekaguliwa, ama kama ni halmashahuri, kama ni mashirika ya umma, kama ni *NGOs* ambazo ni taasisi za kisiasa kama vyama vya siasa, basi wanaweza wakaenda wakatembelea. Vinginevyo hatuwezi kuwa na Taifa ambalo watu wanapewa rasilimali, lakini hawakaguliwi ipasavyo. Tunatengeneza wenyewe mchanganyiko wa kuliangusha Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja iliyowasilishwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Haji.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyo mbele yetu. Mambo mengi yameletwa na mimi nitaenda kwenye maeneo kama mawili matatu hivi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni jambo la wageni. Mheshimiwa Musukuma hapa kachangia vizuri sana na mimi naungana na mchango wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utanzania wetu bado tuna utamaduni wa kutambuana, tuna utamaduni wa kujuana. Kwa hiyo, tunaomba tu uendelee huo utamaduni mpaka hapo tutakapotoka kwenye utamaduni huo. Tuwatambue wageni

wanaokuja Bungeni wanaotoka kwenye majimbo yetu kama ilivyokuwa awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Anatropia anachangia kuhusu watu wa huko nje, sikatai na nakubaliana naye, lakini na wao wana utamaduni wao, wao hata salamu mkikutana *hi, hi* mmeshamaliza, lakini sisi bado tunahitaji kutambuana na kujuana. Kwa hiyo, naomba hilo suala la wageni niungane na Mheshimiwa Musukuma kama alivyochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni jambo ambalo linahusu taarifa mbalimbali hasa taarifa ya *CAG* kwenye kanuni zetu. Labda hili lilitakiwa pia labda lianze na Sheria ya Fedha. Sheria ya Fedha inamtaka Afisa Masuuli apeleke ripoti ya hesabu zake kwa *CAG* mwezi wa tisa, lakini ukiangalia haya inawezekana pia yamewekwa enzi zile tunatengeneza hesabu kwa *manual*, kwa makaratasi.

Mheshimiwa Spika, mimi nime-*practice* kutengeneza hesabu. Unaanza kutengeneza *Financial Statements*, *Balance Sheet*, *Performance, Change in Equity* na mengine kwa daftari. Una-*post* huku unahamisha daftari unatafuta *ledger* una-*post* huku, unahama kwenye *ledger* hii unahamisha kwenye *ledger* nyingine. Sasa haya yalishapitwa na wakati na sasa ni mifumo inayotumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata upelekaji wa hesabu kwa *CAG* kutoka kwenye taasisi pia unatakiwa tu kubadilika. Badala ya mwisho wa mwaka kuwa Juni 30, basi hesabu zilitakiwa kupelekwa miezi mitatu baada ya hapo. Ina maana mwezi wa tisa tarehe 30, sasa hata kipindi pia kinaweza kubadilika. Kufunga hesabu baada ya mwaka wa fedha kumalizika basi wapewe miezi miwili. Badala ya mkaguzi sasa kupelekewa hesabu mwezi wa tisa, basi apelekewe mwezi wa nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mambo yote sasa hivi ukichukua *voucher* umenunua gari kwa milioni tano una-*debt* ya *asset*, una *credit* benki umelipa. Ukishamaliza hapo tayari imeshaji-*set* kwenye *balance sheet*, imeshapeleka kwenye *P and*

*L Account* kama inahitajika kwenda huko, ingawa hiyo haiendi huko. Sasa, kila kitu kitakuwa kimeshamalizika *one the sport* unapo-*post* ile *figure* kwenye mfumo. Sasa hayo yote bado tunasubiri tena miezi mitatu kupeleka taarifa kwa *CAG*.

Mheshimiwa Spika, mimi hili naona tuanze kwenye Sheria ya Fedha kule tuibadilishe, badala ya miezi mitatu hapa tupeleke miezi miwili. Hata mwezi mmoja pia inawezekana na *CAG* sasa afanye ukaguzi wake kwa muda mfupi. Tukifanya hivyo tutaenda tena kubadilisha kwenye sehemu ambayo unatakiwa kupeleka ripoti kwa Mheshimiwa Rais mwezi wa tatu na yenyewe pia inaweza ikabadilika ikarudi hata mwezi wa kwanza au mwezi wa pili, ile ripoti ya *CAG* anapokuwa anaiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukibadilisha hapa, ninataka kwenda kwenye mantiki ya Mheshimiwa Lemburis pale, amezungumzia vizuri kwamba ripoti inatoka lakini kuja kujadiliwa Bungeni inaenda karibu mwaka mzima, miezi karibu tisa ndiyo ije ijadiliwe. Ukikuta kuna taasisi ilifanya makosa na kwa sababu bado haijashauriwa itaendelea kufanya makosa yale yale, yale yale kwa mwaka mzima. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna haja...

**SPIKA:** Nani amesema taarifa?

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, mimi hapa Neema Mwandabila.

**SPIKA:** Aah, Mheshimiwa Simon Songe kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**TAARIFA**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, mimi ninaungana na kaka yangu Mheshimiwa Songe na wote walioongea kuhusu habari ya ripoti ya *CAG*. Ninachofahamu ripoti ya *CAG* inatoka ili Serikali ikaweze kuleta hoja, yaani ikajibie zile hoja. Halafu baada ya hapo ndipo ije itolewe baada ya wao kushindwa au kufanikisha kujibu hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachokifahamu au ninavyoelewa ni kwamba ile inayotoka mapema inakuwa na lengo la kuipa nafasi Serikali ya kutoa/ya kujibia zile hoja ambazo wamezikuta *site*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kuchangia mchango wa kaka yangu kwamba huenda labda ile ripoti muda ule isitangazwe kama inavyotangazwa, ije itangazwe kipindi ambacho Serikali imetoa yaani baada ya kupelekewa ile taarifa ikajibu. Imeshindwa kujibu au imefanikiwa kujibu zile chache zilizobaki ndiyo iende *viral* kwa ajili ya kutuandaa sisi Wabunge kuja kuchangia Bungeni, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe, unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, napata wakati mgumu kupokea kwa sababu alichozungumza ni kitu kingine kabisa, amezungumza namna ya *CAG* anapo-*present* ripoti yake kwa Mheshimiwa Rais, mimi sitaki kuingia huko. Yeye *CAG* ata-*present*, hata akifika tu akakabidhi hivi aah sasa ni yeye.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachozungumza ni ku-*reverse* muda wa kujadili taarifa za *CAG* kutoka hiyo mwezi wa tisa anapopelekewa hesabu, ikianza kubadilika pale ikaja mwezi wa saba akabidhiwe hesabu, ina maana hata kwenye ukaguzi wake wa miezi sita badala sasa ya kwenda mpaka mwezi wa tatu atapunguza kule muda atarudi hata mwezi wa 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akisharudi mwezi wa 12, *point* yangu sasa Bunge linapata nafasi ya kuanza kujadili ripoti ya *CAG* mapema

badala ya ilivyo sasa. Hiyo ndiyo *concern* yangu kwamba ripoti ya *CAG* ianze kujadiliwa mapema Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ninakumbuka mwaka jana kama sikosei nafikiri ulitumia Kanuni ya 5 inayokupa mamlaka wewe kuagiza Kamati zijadili baadhi ya mambo ambapo ni pamoja na utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, lakini haijawekwa vizuri kwenye kanuni zetu kama alivyosema Mheshimiwa Mdee pale. Lazima tuweke utaratibu mzuri wa kurudisha *feedback* ya yale ambayo tunaazimia Bungeni toka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama yatakuwa yana-*hang* maana yake hata Maafisa Masuuli hawatachukua *serious* mambo ya uwajibikaji kwenye maeneo ambayo tunaazimia kama Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupe mfano mdogo, Bunge linaazimia magari ambayo yamepita muda yatolewe yauzwe, jambo dogo tu! Wanaomba kibali taasisi Wizara ya Fedha inakaa siku 191, miezi sita. Kuna haja gani ya kukaa miezi sita kutoa kibali ya yale magari kutoka kwenye maeneo husika? Lakini wakijua kwamba Bunge baada ya miezi mitatu litahitaji kupata utekelezaji wa maazimo, maana yake watafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine, maazimio ya Bunge yametoka taasisi fulani haina hati ya eneo itafute hati ya eneo. Inakaa miaka mitatu haijapata hati. *Are we serious?* Miaka mitatu hamjapata hati! Wizara iliyopewa maelekezo nichukulie ni Wizara X, halafu hati zinapatikana kwenye Wizara ya Ardhi. Unaenda kwa miguu unapata hati. Sasa kwa nini tunachukua miaka mitatu? Ni kwa sababu hakuna kanuni inayowataka kwamba baada ya Maazimio ya Bunge kutoka, miezi mitatu mlete maazimio Bungeni yaende kwenye Kamati, na kama kuna dosari yarudi Bungeni yaamuliwe upya na kama kuna jambo ambalo linatakiwa lifanyike basi linafanyika kwa utaratibu wa ile kanuni kama itakavyokuwa imeongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukifika hapo tutakuwa tumefika pazuri na watu, Maafisa Masuuli na Afisa Masuuli watafanya kazi wakijua

kwamba baada ya miezi mitatu, baada ya miezi sita ripoti ya maazimio ya Bunge inarudi tena Bungeni. Naamini watafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, lakini mimi naomba nichangie maeneo mawili tu; kwanza ningependa kuliomba Bunge lako tutathmini juu ya siku ambazo tunakwenda kukagua miradi. Kwa sababu, kwa mujibu wa kanuni kama sikoseni nadhani ni siku zisizozidi saba.

Mheshimiwa Spika, sasa nikitoa mfano wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo yenyewe ina Wizara tatu na hizi Wizara tatu zimetawanyika *almost* nchi nzima, kwa hiyo, vinginenvyo tunashindwa au tutashindwa kutekeleza wajibu wetu wa kuisimamia na kuishauri Serikali. Kwa hiyo, kwenye hili, ombi langu nadhani tuone namna gani siku hizi zinaweza kuongezwa kwa sababu kwa kweli siku zilizopangwa hazitoshi kabisa kabisa. Na tunaandika sehemu ndogo sana ya ukaguzi wa maeneo kwa sababu ndiyo siku zilizoturuhusu na ndivyo tulivyokwenda. Kwa hiyo, ningeomba kwenye hili tutafute namna gani ya kuongeza siku hizi ili Kamati hizi ziweze kufanya kazi yake kwa mujibu wa Katiba inavyoturuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili hili ni ombi; pamoja na kwamba hali zetu uchumi haujatengemaa, lakini naendelea kuwaangalia Wabunge jinsi wanavyopata tabu namna wanavyosafiri. Wabunge wanaosafiri kwenda kutembelea maeneo mbalimbali, kwa mfano wako watu wanatoka Dodoma wanakwenda mpaka Mtwara, siku zimepangwa tatu au nne. Kwa hiyo, maana yake siku tatu ni za kusafiri siku moja ni ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba tuangalie namna gani Wabunge hawa wanaweza kusafiri, lakini ufumbuzi wake

utapatikana kwamba kama tunaweza tukaongeza idadi ya siku ili iwape muda angalau wa kupumzika, kwa sababu unapomtoa Mbunge hapa unampeleka Mtwara kwa siku tatu maana yake huyu anapofika kule anatafuta nafasi apumzike tu. Hana nafasi ya kufanya kazi navyopaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mwingine, Kamati yetu iliondoka hapa kwenda Kagera kwenda kukagua maeneo maeneo fulani. Waliondoka hapa na basi walifika kule wote ni ..., kwa hiyo, ningeshauri tuangalie. Lakini mfano mwingine wakati Wabunge wale walipokwenda kenye mambo ya michezo, wamechoka sana wale Bunge. Mungu tu atubariki, lakini hata tunapofika kule tunakuwa kama watoto yatima vile na sijui tunakwenda kufanya ... *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu tutafute namna gani Wabunge tutawasafirisha kwa sababu kumpata Mbunge mmoja ni shughuli na Serikali inalipia na chama chetu kinalipia. Kwa hiyo, ningeomba kama itawapendeza tutafute namna gani ya kuwasafirisha Wabunge wetu kwa salama na amani kwa sababu tunavyowasafirisha ni *risk* kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako wachache wanaweza kupata kuongozwa, lakini wengi hawaongozwi. Kwa hiyo, ningeomba tulitafakari hili na tuone tutawasafirishaje Wabunge wetu kwa salama ili waende kwa salama na warudi kwa salama, lakini wakiwa na heshima zao kama Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, sasa ni wakati wa Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kuja kuhitimisha Hoja ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KANUNI ZA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa hoja na sasa kuhitimisha, lakini vilevile, niwapongeze

Wabunge kwa michango mizuri sana yenye tija na yenye afya katika Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza michango, michango mingi ambayo yameigusa moja kwa moja azimio nimeona tofauti au kidogo kuna marakebisho au kuna mapendekezo kwenye suala la utambulisho wa wageni, ambalo limezungumzwa karibu na Wabunge wote. Kuna baadhi ya Wabunge wamesema ni kweli Wabunge ni wengi, kuna Wabunge wamesema ni utaratibu wa *Commonwealth*, lakini *of course* tuna tofauti za *culture* za *Commonwealth*.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama kwenye Bunge la Uingereza kuna Mbunge analeta wajumbe 300 kutoka kwenye *constituency* yake kuja kuwatambulisha kwenye Bunge. Hakuna kitu kama hicho, na hawana utamaduni kama huo na wao vilevile utamaduni wao wana-*communicate* na Wabunge wao kwa *email*, hata kuonana nao inakuwa hawaonani, lakini sasa hapa ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi hili na nimesikiliza mawazo, kwa hiyo nitalielekeza tena kwenye utawala walipokee, waende wakalifanyie kazi na kulitizama namna gani. Hili lilisemwa na Mheshimiwa Francis, Mheshimiwa Sanga yeye aliunga mkono kuwa watu ni wengi, lakini tutizame na *culture* yetu lakini tutalipeleka kwenye Kamati yetu ya Utawala walifanyie kazi na baadaye kuwe na ..., hii *reservation* itizamwe tena kwa sababu ya umuhimu na *culture* zetu ambazo tunazokwenda nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mavazi tunazo kanuni; Kanuni ya 173 imeeleza vizuri kabisa kuwa mavazi haya ya Kibunge na kwenye Kamati yaende sawa na vilevile imeleta unadhifu kwenye Kamati. Ni kweli, hata humu ndani kuna watu wanaingia hawavai soksi. Wamo na nikiwanyanyua sasa hivi mtaona wamevaa hawana soksi, kwa hiyo si jambo jema. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge ni sehemu ambayo ina heshima yake, mavazi siyo soksi tu tutavaa kule Ilala, tutavaa maeneo mbalimbali lakini hapa tujaribu kuwa nadhifu, ndio inakufanya na

wewe hata matamshi yako au michango yako yanaendana na namna ulivyovaa. Kwa hiyo hilo nimelitoa litakuwa kwenye kanuni ya 173 iseme nini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mageni yeye kataka suala la wageni libaki *of course* tushatoa maelekezo *reservation* ambao nani watatusaidia kama ni utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahadi ya uzalendo imepokelewa ni jambo muhimu sana, Wabunge tukumbuke tupo kwenye Taifa ambalo linakwenda mbele sana, linahitaji uzalendo wa pamoja, kuchangia kwa uzalendo, lakini kuonesha mambo ambayo sio mazuri vilevile Wabunge wawe na fursa ya kuweza kuonesha hayo mambo ambayo yanakwenda ambayo si ya kizalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spiska, kuna nani, Mheshimiwa Anatropia, aliendelea pia kusema kuhusu wageni wapite, hakuna mgeni anayekatazwa kuja Bungeni, wageni wanaruhusiwa kwa taratibu, wakifuata taratibu, *this is a public entity complex*, ni jengo la wananchi, hakuna mwananchi anayekatazwa ilimradi afuate taratibu tu kwa sababu hili ni eneo vilevile lina *security conscious*. Ni eneo la kiusalama, huwezi kuruhusu watu kuingia tu bila kutizamwa ni nani, ajitambulishe, awe na kitambulisho na ninyi mmeona Mabunge mengine nchi zote tena wako *very strict* zaidi yetu sisi.

Mheshimiwa Spika, kuna Wabunge hapa wanalalamika kukaguliwa, haiwezekani uingie humu ndani usikaguliwe, pamoja na uzalendo wako hujui umeamka na nani na wengi tunajua tunamka na wengine watu tofauti kwenye vyumba vyetu, hujui mtu anakuwekea nini kwenye begi lako. Kwa hiyo, hili suala la usalama ni *very important* na ni sahihi, mimi napongeza vyombo vyetu vya usalama Bungeni kwa namna wanavyofanya kazi kwa utiifu na uadilifu na hii ndio Taifa linavyokuwa. Vyombo vya usalama vina sehemu yake, Wabunge wanasehemu yao, kila mtu aheshimu eneo linalo nini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna kipindi hapa Bunge lililopita, kuna Mbunge alikuja na gari mlango huu hapa huu mkubwa karibu na benki zetu, kila akikaguliwa lile gari linaonesha alamu kuwa kuna kitu sio sahihi, mpaka wakaletwa wale wanyama ambao wanakazi na *training* ya kukagua dawa, silaha, baruti bado wakawa na mahofu nayo. Mwisho wakakuta kuna kitu, usalama ule wa Mbunge, usalama ule wa Wabunge na usalama ule wa Taifa letu. *(Makofi)*

Kwa hiyo niwaombe Wabunge, wageni wanaruhusiwa kuja lakini masuala ya kiusalama lazima tuzingatie, lazima hilo halina mjadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Noah, yeye kazungumzia masuala ya Wabunge. Saa nyingine kunakuwa na muda, muda wa dakika tano tunatoa Wabunge wanapokuwa wengi kwenye Wizara moja. Wizara moja tumeshakuta hapa tunakaa kwenye Kiti tunapata Wabunge sio chini ya 90 kwa siku mbili una-*manage* vipi *time?* Yapo maeneo tuna-*manage time*, yapo maeneo ambayo tunaruhusu muda, kuna Wabunge hapa wanaomba muda niongezee dakika moja Mheshimiwa Spika, wanapewa lakini tuzingatie vilevile kanuni na maelekezo yetu ni Mbunge atachangia kwa muda usiozidi dakika 10, haikusema dakika 10. Kwa hiyo, Kiti kikitizama unaanza kupuyanga puyanga kinakupa dakika mbili tu. Hiyo nimechomekea tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ripoti ya *CAG* inapokuja Bungeni, anapokabidhiwa Mheshimiwa Rais ni *opinion* ya *CAG,* lakini bado haijapata fursa Serikali kupewa muda na wao kujibu, sasa shida inakujaje unapoona ripoti, ripoti hii haipoi, shida inakuja ripoti inapoletwa Kamati zinahusika na ripoti hii *PIC* ya *PAC*, Kamati za fedha za *LAAC* zote zinakuwa na majukumu ya kipindi cha bajeti, tumeelewana Waheshimiwa Wabunge? Kipindi kile *accounting officers* ambao ni Makatibu Wakuu ndio wanatakiwa kuja kujibu na wao wanaandaa bajeti za Wizara zao. Kwa hiyo kipindi hiki kinakuwa kigumu kui-*fast track* ripoti ya *CAG* ili sasa iweze kuwa moto, ripoti ya *CAG* inaheshimika, inafanyiwa kazi, lakini Serikali lazima wapewe muda na wao kuja kujibu. Tumepokea hayo mapendekezo, utawala tutawaomba nao waifanyie kazi

kutizama namna gani bora ya kuweza kuhakikisha kuwa hizi ripoti zinakwenda kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Halima Mdee, kazungumza kitu ambacho na yeye pamoja na *CAG* haikuwemo kwenye azimio hili, haya ni mambo ambayo Wabunge wameona ni bora wayaguse na mimi nayapeleka tena kwenye utawala watizame namna gani wataweza kuya-*fast track* vizuri.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema azimio la Mheshimiwa Halima Mdee, pamoja na Wabunge wengine kuna mambo ambayo hayamo kwenye mjadala, *primary* mjadala wa leo, lakini ni maoni muhimu na tunachukua tutakabidhini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Musukuma, amezungumzia kuhusu suala la *VIP* ni kweli limewakerakera Wabunge, lakini utawala wameliona na Bunge lijalo kutakuwa na mabadiliko kwenye suala hili, nafikiri mtaona namna Bunge linavyo nini. Mheshimiwa Musukuma, ameomba tu utaratibu wa kizamani, *of course* tushatoa maelekezo, utawala watalifanyia kazi tena kuli-*visit* hili na kutizama namna gani wateweza kuendana vizuri na shughulli za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nalo nilishazungumzia kuhusu muda dakika 10, Mheshimiwa Tarimba ame-*support* suala la uzalendo ambalo ni muhimu sana na Mheshimiwa Sendeka amesema tuongeze tuweke kipengele cha adhabu, mtu ajijue akikosea anapewa adhabu, namna gani atavyoshughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, masuala ya bendera ni kweli kuna kero, leo Dar es Salaam pale Wabunge 200 kila mtu na bendera yake hao *traffic* nafikiri nao watazimia siku hiyo. Kwa hiyo, mimi nafikiri suala la bendera hili kwa maeneo ambako kama mikoa mikubwa kama Dodoma, Zanzibar, Dar es Salaam, Arusha wapi Mwanza hili tuache utawala walifanyie kazi na watupatie majibu yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mavazi ya asili, tulishawahi kuona humu ndani Wabunge wengi, humu ndani kuna kipindi kuna baridi

wanavaa mavazi *of course* wanavaa nguo za kawaida, lakini juu anajifunika kuna ile nguo maalum na hasa kama ile nguo ya kina Sendeka ile ambayo ina heshima yake na inaruhusiwa sababu na mazingira unayaona kuna baridi na mtu kaamua kujifunika, tunachokiona hapa Wabunge, sitaki kumtaja sasa hivi kastaafu miaka mingi mara nyingi yeye akiingia anaingia nayo, lakini kuwe na staha, kuwe na staha. Kitu muhimu kwenye Bunge ni staha, ujiheshimu na uheshimu hicho ulichokivaa, lakini ujue uko na wenzio humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, katoa hoja muhimu za *CAG*, ni kweli kama ulivyosema *CAG* analeta *opinion* yake, baadaye Serikali inapata fursa ya kukaa na Kamati na kuweza kujibu lakini ni kweli watuhumiwa au watu wanaobainika wanafuja, wanafanya fujo kwa pesa za umma lazima wachukuliwe hatua, lazima.

Mheshimiwa Songe amezungumzia wageni kutambulika, yeye kasema anaunga mkono na ndio kipindi hiki hasa cha kuwaleta wageni wengi tunaona sasa hivi Wabunge, ndio *culture* zetu za Kitanzania, kwa hiyo watajaribu kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la *CAG* tushalisema, nani ma-*accounting officer* wanakuwa na muda, wanashughulikia bajeti kipindi wakati ripoti inakuja. *Oversight committee* nazo zinakuwa kwenye bajeti, kwa hiyo hakuna muda wa kujigawa kukaa na *CAG* na *accounting officers* na kutoa maamuzi ya hoja wakati vilevile kuna hoja za bajeti.

Mheshimiwa Neema yeye amezungumza hilo hilo kwa *CAG* yeye na-*trigger* tu jicho la Bunge. Mheshimiwa Zahor amezungumzia siku ni chache, sasa siku hizi Bunge lina muda wake, kuna mikutano minne ya mwaka, lakini kuna muda kuna siku zake, kuna *implication* za gharama. Kwa hiyo, hili sasa litatizamwa na nchi yetu sasa tunakwenda kwenye uchumi mkubwa huko mbele Utawala na Spika, atakayekuwepo atalitazama na kutazama kuongeza fursa zaidi kwa Wabunge kuweza kufanya ziara zaidi na kuweza kutizama maeneo muhimu kwa ufanisi na kwa siku zinazotosha.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi mimi nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri ambayo kwa kweli imeonesha ukomavu wao. Mimi niwaombee tu la kila la heri kwa Bunge lijalo likija na ninyi mrudi, muendelee kusaidia Taifa letu, muendelee kusaidia wananchi wetu, kuendelea kusaidia Rais wetu kufanikisha azma yake ya R zake nne, lakini kujenga umoja wa Taifa letu bila kubaguana kabila, rangi, dini. Kila mtu na dini yake, kila mtu akae na dini na imani yake, ile dini kama ya watu wengine ambayo ya kuvuavua nguo hizo kwa kweli hazitaruhusiwa sababu si maadili ya kumuabudu Mungu kwa kutokuwa na mavazi, kukaa uchi, huyo atakuwa ni mchawi huyo na huyo mchawi atakuwa anatoka nafikiri kwa Mheshimiwa Kingu kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, kwa ruhusa yako naomba sasa kusoma Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kufanya Marekebisho au Mabadiliko katika Kanuni za Bunge, imetolewa chini ya Kanuni 176(1) na (2) ya na fasili ya 3(3)(e) na Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya Kudumu za Bunge, toleo la Februari 2023.

Kwa kuwa, upo utamaduni wa Mabunge Jumuiya za Madola kufanya maboresho ya mabadiliko katika kanuni zinazotumika kwa ajili ya kutumiwa wakati wa Bunge linalofuata;

Na kwa kuwa katika Bunge hili zimekuwa zikijitokeza changamoto za mara kwa mara za matumizi ya tafsiri wakati wa uendeshaji wa shughuli za Bunge;

Na kwa kuwa kumejitokeza uhitaji wa kuweka kwenye kanuni baadhi ya masuala mapya ya kibunge kwa ajili ya kuboresha na kuweka usimamizi mzuri wa shughuli za Bunge;

Na kwa kuwa kamati za Kanuni za Bunge, ilifanya uchambuzi wa changamoto za matumizi ya kanuni na kutafakari maeneo mapya yanayohitaji kuweka mashariti ya kanuni;

Na kwa kuwa Kamati ya Kanuni imeona umuhimu wa kufanya maboresho au marekebisho na kwa kuwa kanuni ya

137(3)(e) na nyongeza ya nane ya kanuni inaipa mamlaka Kamati ya Kanuni kujadili na kutoa mapendekezo juu ya kufanya marekebisho au mabadiliko katika kanuni;

Na kwa kuwa Kanuni ya 176(1) na (2) inaipa Kamati mamlaka ya kuwasilisha Bungeni mabadiliko ya Kanuni za Bunge kwa njia ya azimio;

Na kwa kuwa Kanuni ya 178 imetoa mashariti kwamba, baada ya kupitisha Azimio la Bunge la mabadiliko ya kanuni, kanuni zinazotumika zitafutwa.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Mapendekezo Marekebisho ya Mabadiliko ya Kanuni za Kudumu za Bunge kama ilivyowasilishwa kwa mujibu wa Kanuni 137, 176, 178 za Kanuni za Bunge Toleo la Februari 2023 yanapitishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kabla sijawahoji nimepokea mapendekezo hapa ya marekebisho ya hizi Kanuni, nimepokea marekebisho kwenye Kanuni ya 139 ili tuongeze fasili hapo ambayo inahusu mabadiliko haya yanayohusu mchango uliotolewa na Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

Kwa hiyo, itaongezeka kanuni ndogo badala kuishia kanuni ndogo ya 19 ama fasili ya 19 itaishia fasili ya 20, kwa hiyo hapa baada ya 16 itaongezeka nyingine, baada ya kumaliza 16 ambayo inazungumzia; "Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya 15 Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za

Mitaa zitawasilisha taarifa kuhusu hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma itawasilisha taarifa kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma katika Mkutano wa Bunge wa mwezi Oktoba - Novemba."

Baada ya Kanuni ndogo hiyo itaongezeka kanuni itakayokuwa inasema; "Serikali italazimika kuleta utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatakayotokana na taarifa zilizowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya 16 kwenye Bunge la Januari – Februari na Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa zitawasilisha taarifa Bungeni, isipokuwa kwamba katika kila Mkutano wa Bunge, Kamati hizi mbili zitapewa nafasi ya kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge." *(Makofi)*

Kwa hiyo, haya ndio marekebisho ambayo yataongezeka hapa Waheshimiwa Wabunge na kwa sababu hoja nyingine ameshafafanua Mheshimiwa Naibu Spika kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati, sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge, wanaoafiki Azimio la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni za Bunge kuhusu marekebisho ya Kanuni za Bunge.

*(Azimio la Kamati ya Kudumu ya Bunge za Kanuni kuhusu Marekebisho za Kanuni za Bunge Lilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Haya, mmoja tu ndio amesema sio, kwa hiyo wengi mmeafiki kwa hivyo kanuni zetu zimepitishwa rasmi na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kwanza kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ya Kanuni za Bunge kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa niaba yetu sote na kwa mapendekezo ambayo wameyaleta na kisha leo Bunge limeweza kuyaridhia basi *In Shaa Allah* tunawatakia kila la heri wale ambao Mwenyezi Mungu atawajaali, kuja kuzitumia kanuni hizi muda wake utakapofika. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu kwa utaratibu wetu wa Kibunge, hoja hii huwa anawasilisha Naibu Spika na ameshatoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge mlikuwa

mmeshazisema hapa ndani kwa kifupi kabisa kuna baadhi ya hoja zilisemwa hapa ikiwa moja wapo ni kuhusu ukaaji Bungeni, kulikuwa na mapendekezo ya nani akae wapi. Sasa pamoja na kwamba kanuni zetu huwa zinasema ukaaji ule wa jumla, lakini yametokea mapendekezo hapa ambayo tumeyachukua, tutajaribu kuona namna bora ya kuyafanyia kazi.

Jambo lingine ambalo limeelezwa kwa kirefu kabisa na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu muda wa uchangiaji, kanuni zetu zimeweka muda maalum wa uchangiaji, lakini sasa kwa sababu pia kama mnavyofahamu Wabunge tunaenda kuongezeka, kwa hiyo, kutakuwa na changamoto kubwa zaidi inayohusu muda.

Sasa kuna pendekezo ambalo limetolewa hapa kwamba pengine tupunguze ule muda wa mapumziko ama ule muda ambao tunapumzika kuanzia saa saba mchana na Bunge kurejea saa kumi na moja. *(Makofi)*

Niseme wazo hilo limepokelewa, lakini kwa sababu hatukupokea sasa yale marekebisho ya moja kwa moja, kwa hiyo, halijafanyiwa marekebisho, lakini nieleze tu kwa kifupi kwamba ule muda ulitolewa sio kwamba mtu atatoka hapo aende kimsingi akapumzike labda, ilikuwa inatolewa muda ili Mbunge kipindi hiki anachokuwepo hapa Bungeni aweze kupata muda wa kwenda kwenye ofisi hizi za Serikali kufuatilia hoja za wananchi ambazo anakuwa anazo na pengine ndio hiyo inayosababisha siku hizi sasa Wabunge hata muda ambao huwa wanashauriwa kwamba msije huku upande wa Serikali ili hawa wa Serikali wapate kusikiliza hoja za Waheshimiwa Wabunge, Wabunge sasa wanatumia muda wa Bunge kuja kuzumgumza na upande wa Serikali kimsingi ule muda uliokuwa umetolewa wa mapumziko wa kuanzia saa saba mchana mpaka saa kumi na moja ulitolewa ili ofisi za Serikali zisiwe zimefungwa, Mbunge aweze kwenda huko, afuatilie haya na haya ambayo yanahusu mambo ya jimboni kwake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wakati tukitafakari juu ya jambo hili na kama tutaona kwamba bado kuna haja ya kubadilisha huo muda

kwamba muda wa mapumziko uwe ni mfupi kuliko muda ambao tunautumia sasa, basi hayo nayo yatazamwe kwa mapana hayo kwa maana ya kwamba Mbunge anatarajiwa sio tu kuwasilisha hoja za wananchi hapa ndani, lakini pia kwenda kufuatilia kwenye hizo ofisi zinazohusika. Kwa hiyo, ndio nia hasa ya kuweka ule muda ambao umewekwa pale.

Sasa mwingine ni muda ule wa taarifa pia umechangiwa sana hapa kwamba muda unamalizwa na yule mtoa taarifa, nafikiri ni jambo ambalo Bunge lijalo kutakuwa na uwezekano na uzuri Katibu yupo hapa, mafunzo yataendelea kutolewa kwa sababu imetokea kipindi hiki kwamba taarifa zinazotolewa si taarifa zile ambazo kwa kweli ni taarifa za kibunge, mtu anatoa taarifa kwa sababu yeye anataka kuchangia, anasema jambo hili na jimboni kwangu lipo, ile inakuwa sio taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ni kwamba yule anayesema kile lazima umpe nafasi amalize hoja yake ili ujue kuna jambo amelisahau, kuna jambo amelikosea. Sasa mtu yupo katikati ya sentensi taarifa, kwa sababu na wewe umesikia tu kuna jambo ambalo amelitaja na wewe unataka ulisemee, sasa hiyo kidogo ndio ambayo inatupa changamoto, lakini maana halisi ya kanuni hii ni kutoa fursa kumrekebisha Mbunge ambaye pengine anakosea jambo fulani, ama kumuongezea taarifa kama kuna jambo amelisahau. Sasa kama atakuwa hajamaliza kale kahoja yaani tuseme ile sehemu ya mtiririko wa hoja yake kama hajamaliza hata sehemu akahamia hoja nyingine halafu wewe unasema taarifa, maana yake hujui kama ndio sentensi iliyokuwa inafuata ama ni sentensi ambayo yeye amejipanga kuwa ya pili, wewe umeshaingia hapa ndani unasema taarifa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hiyo ndiyo inayoleta changamoto, kwa hivyo tutajitahidi kuwekeza kwenye eneo la elimu ili mtu asitumie muda wa Mbunge, mwenzake kumpa taarifa kwenye jambo ambalo kwa kweli yeye asingeweza kuchangia habari ya jimbo lako wewe, asingeweza kuchangia hoja ambayo ipo kichwani kwako wewe, lakini kwa hoja ile aliyonayo kama unamuongezea taarifa ndio maana unatumika muda wa Mbunge. Haya yote

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kuyafanyia kazi ili Bunge letu liendelee kufanya kazi kwa ufanisi.

Sasa yameelezwa hapa mengine ni haya ya mzunguko wa taarifa ya *CAG*, hili nalo tumelipokea japo sio jambo la kikanuni, ni jambo la kisheria na kwa sababu sisi ndio watunga sheria tulishaanza mazungumzo na *CAG*, ajaribu na yeye kutazama kwa sababu wale pia Wakaguzi wa Ndani utendaji wao wa kazi na nini na taarifa namna anavyozipokea, basi ule muda kadri unavyopungua na teknolojia imeongezeka sana hakuna sababu ya kusubiria taarifa ya mwaka mzima ije baadaye wakati inaingizwa humo na inakuwa ipo. Kwa hiyo, hata wale wa upande wa *CAG* wanao uwezo wa kuendelea kuzitazama hizo taarifa kadri mwaka unavyokwenda.

Kwa hiyo, nafikiri kadri muda unavyoenda na teknolojia inavyozidi kukua, muda utaendelea kushuka na kwa hivyo hoja zilizozungumzwa nanyi Waheshimiwa Wabunge, hakutakuwa na kusubiri mwaka mzima ili hatua ziweze kuchukuliwa kwa wakati kwenye hoja ambazo zinakuwa zimeibuliwa na taarifa ya *CAG*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nyingine sasa kuhusu ufuatiliaji nadhani tumeshaweka sasa vizuri kanuni zetu kwa maana ya kwamba tukishajadili kwenye Bunge la Oktoba – Novemba basi ile taarifa sasa Bunge linapokuja lile la Januari tayari Serikali inatakiwa kuleta taarifa kwamba imefikia wapi utekelezaji wa yale maazimio, halafu yale ambayo sasa kwa sababu yale maazimio pia huwa yanakuwepo ya muda mfupi, ya muda wa kati na muda mrefu, yale ambayo yanakuwa muda mrefu ndio ile sehemu ya pili ya haya marekebisho ambayo sasa Kamati hizi zitakuwa zinapewa nafasi ya kueleza jambo hili limeshatekelezwa kwa asilimia fulani, jambo hili limetekelezwa kwa asilimia fulani, jambo hili bado linafanyiwa kazi. Kwa hiyo, maana yake ufuatiliaji utakuwa kila Bunge tunapokutana, maana yake lile wazo la kutoa kama taarifa hivi ndani ya miezi mitatu maana yake watakuwa wanajua kila Bunge linapokuja litakuwa na taarifa ya utekelezaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yametolewa mawazo hapa kuhusu kiapo; kuhusu viapo vile sasa ambavyo tutakuwa tunavyo kwenye kanuni na kwamba adhabu gani itakuwa inatolewa, sasa hayakuletwa hapa marekebisho kwamba ni adhabu gani itolewe, lakini nadhani ni jambo pana sana ambalo Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kutafakari ni namna gani tutaweza kumthibitisha mtu huyu amekiuka kiapo hiki au amekiuka maelezo haya. Kwa hiyo, hayo yote tuendelee kuyatafakari kwa mapana wakati tukijaribu kuweka mazingira mazuri zaidi ya watu kuwa wazalendo kwa Taifa lao, lakini kujua kwamba kazi ambayo wametumwa na wananchi hapa ni kazi kubwa na ni kazi nzito, kwa hiyo lazima watangulize utaifa mbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, basi huo ndio ulikuwa ufafanuzi kwa kifupi kwa ajili ya kuongeza yale ambayo Mheshimiwa Naibu Spika ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii alikuwa ameshatoa ufafanuzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo sasa kanuni zetu hizi kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria zitaenda kuchapwa kwenye Gazeti la Serikali kisha zitaanza kutumika Bunge lijalo na siyo Bunge hili linaloendelea sasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliopo hapa Bungeni; wageni 23 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Wenyeviti wa Wanawake na Watoto wa Dayosisi za KKKT kutoka mikoa mbalimbali nchini, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni 31 wa Mheshimiwa Flatei Gregory Massay ambao ni Wakuu wa Shule za Msingi Mbulu Vijijini, Mkoani Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa nne wa Mheshimiwa Muharami Mkenge ambao ni ndugu zake kutoka Kaskazini Pemba, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndio yalikuwa matangazo ambayo nilikuwa nayo hapa mbele, basi baada ya matangazo hayo niwashukuru kwa kazi nzuri ambayo tumeweza kuifanya siku

ya leo na sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.26 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 12 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*